# Nipashe

Jumamosi Januari 15, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580826

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





**O Yeong-su won wa Squid Game kuwania tuzo**

UKURASA 14


SportPesa

TZS. 846,297,200

NI YA KWAKO WIKI HII, BETI LEO UWE MILIONEA

SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#




**Bashungwa** awaonya wanaotoza michango uandikishaji watoto

UKURASA 9



# Ukame waua mifugo 62,000

UKURASA 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**MISRI YAIPA TANZANIA VIFAA TIBA MAMILIONI**

WIZARA ya Afya, imepokea msaada wa dawa na vifaa tiba vyenye...

UKURASA WA 3

**NAMBA MSHITAKIWA KESI MBOWE YADAIWA KUUZWA**

WAKILI wa utetezi katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti...

UKURASA WA 4

**CCM YATISHIA KUZIFUTA SHULE JUMUIYA WAZAZI**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimetishia kuzifuta shule za Jumuiya za...


## Vigogo zaidi CCM wapigana vikumbo uspika

UKURASA 3



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya (kushoto), akiteta jambo na mmoja wa mawakili wa utetezi, Fridolin Bwemelo, kabla ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha jana, kumkuta na kesi ya kujibu na wenzake sita katika shauri la uhujumu uchumi namba 27 linalowakabili. **PICHA: ALLAN ISACK**

# Mashahidi 10 kumtetea Sabaya baada ya kuwa na kesi ya kujibu

UKURASA 2


**MICHEZO** **CHAMA: NIMERUDI NYUMBANI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan, akipokea Ujumbe Maalumu kutoka kwa Rais Evariste Ndayishimiye wa Burundi uliowasilishwa na Mjumbe maalumu ambaye pia ni Waziri wa Masuala ya Afrika Mashariki, Vijana, Michezo na Utamaduni, Balozi Ezechiel Nibigira, baada ya kuwasili Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Ukame waua mifugo 62,000

**Na Jaliwason Jasson,** SIMANJIRO

UKOSEFU wa maji na malisho kulikosababishwa na ukame Simanjiro mkoani Manyara kumesababisha vifo vya mifugo 62,593 katika vijiji mbalimbali.

Mifugo iliyokufa kutokana na ukame huo ni ng'ombe 35,746, kondoo 15,136, mbuzi 10,033 na punda 1,670.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Sendeu Laizer, alisema hayo jana wakati akiwasilisha taarifa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo.

Laizer alisema kwa sasa hali ya mifugo katika maeneo mengi ya Simanjiro si ya kuridhisha kutokana na mifugo mingi kufa kwa sababu ya uhaba wa maji na malisho. Alisema hali hiyo imesababishwa na ukame.

Hata hivyo, alisema kwa sasa halmashauri inaendelea kukusanya taarifa za vifo vya mifugo vilivyotokana na athari za ukame.

"Kuwapo kwa hali ya ukame kumesababisha baadhi ya mifugo kufa na wafugaji wengi kuhama na kurundikana katika maeneo machache yenye maji na malisho, wakijaribu kuokoa mifugo yao," alisema. Akizungumza na Nipashe kuhusu hali hiyo, Laizer alisema: "Tangu Novemba, mwaka jana hadi sasa, mvua hazijanyesha. Hali si nzuri kabisa. Tangu mvua za masika ziliponyesha, hadi sasa hakuna mvua".

Alisema vijiji 40 kutoka kata 11 vimekumbwa na ukame na kwamba mifugo mingi imekufa na mizoga kutapakaa mitaani.

Laizer alisema kutokana na hali hiyo, Halmashauri imeshawasiliana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki na Naibu Waziri, Abdallah Ulega, ambao wameahidi kuwa watafanya ziara ya haraka wilayani hapa leo.

Pia alisema halmashauri imeshawasiliana na Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk. Suleiman Serera, ili kuratibu shughuli ya maombezi maalumu ya mvua itakayoongozwa na viongozi wa mila na dini.

Kutokana na hali ya ukame, Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, alisema jamii nyingi zimeingia kwenye umaskini kutokana na mifugo yao kufa. Alisema kwa sababu ya ukame uliopo nchini, baadhi ya wafugaji wamehamisha mifugo yao nje ya nchi ili ipate malisho.

Naye Diwani wa Naisinyai, Taiko Kurian, aliomba serikali kuruhusu mifugo kuingia ndani ya ukuta wa madini ya tanzanite ili kupata malisho.

"Mifugo ni benki ya jamii za kifugaji. Sasa inapokufa kwa ukame inakuwa tatizo. Tunaiomba serikali iruhusu mifugo kuingia ndani ya ukuta wa madini ya Tanzanite kwani haitaathiri," alisema.

# Misri yaipa Tanzania vifaa tiba mamilioni

**Na Mary Geofrey**

WIZARA ya Afya, imepokea msaada wa dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 864 kutoka serikali ya Misri kwa ajili ya mapambano dhidi ya magonjwa mbalimbali.

Msaada huo ulipokewa jana jijini Dar es Salaam katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi, kutoka kwa Balozi wa Misri nchini, Mohamed Gaber Abouelwafa.

Prof. Makubi alisema msaada huo umeletwa baada ya ziara ya kikazi ya Rais Samia Suluhu Hassan, nchini Misri Novemba, mwaka jana.

"Tunamshukuru sana Rais Samia pamoja na Serikali ya Misri kwa kushirikiana na Tanzania hasa katika kuboresha sekta ya afya kwa kusaidia mahitaji mbalimbali ikiwamo upatikanaji wa dawa na vifaa tiba," alisema Prof. Makubi.

Pia alisema msaada huo utawasaidia wananchi wenye uhitaji katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya nchini.

Naye Balozi wa Misri nchini Tanzania, Mohamed Gaber Abouelwafa, alisema kujitoa kwa serikali ya Misri kusaidia sekta ya afya ni kutokana na jitihada za Rais Samia katika kuwaletea maendeleo wananchi, ikiwamo kuboresha sekta ya afya.

"Serikali ya Misri itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kusaidia maendeleo ya Watanzania hasa katika kuboresha sekta ya afya. Hii inatokana na nia njema ya Rais Samia katika kuleta maendeleo kwa wananchi, hususani katika kuboresha sekta ya afya," alisema Balozi Abouelwafa.

# Mashahidi 10 kumtetea Ole Sabaya, ana kesi ya kujibu

**Na Allan Isack, ARUSHA**

UPANDE wa utetezi katika kesi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, unatarajiwa kupeleka zaidi ya mashahidi 10 na vielelezo kadhaa kujaribu kumnusuru kufungwa tena.

Mashahidic hao wa utetezi watapanda kizimbani baada ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, kumkuta Sabaya na wenzake sita kuwa wana kesi ya kujibu.

Sabaya na wenzake wanakabiliwa na mashtaka matano ya uhujumu uchumi yakiwamo kuongoza genge la uhalifu, kujihusisha na vitendo vya rushwa, matumizi mabaya ya madaraka na utakatishaji wa fedha.

Mbali na Sabaya, washtakiwa wengine ni Sylvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya(31).

Wakili upande wa utetezi, Mosses Mahuna, aliieleza mahakama hiyo kwamba watakuwa na mashahidi wasiopungua 10 pamoja na vielelezo vya ushahidi na washtakiwa watajitetea kwa njia ya kula kiapo.

"Kwa kuwa siku hii ndiyo tumepata uamuzi huo mdogo, tunaomba muda wa kujiandaa na kuwaandaa mashahidi wetu. Pia tunaomba mahakama kutupa nafasi ya kuahirisha kesi hii na kutupangia tarehe nyingine kwa washtakiwa kuanza kujitetea," alidai Wakili Mahuna.

Naye Wakili wa Serikali Mwandamizi, Janeth Sekule, alidai kwamba hawana pingamizi na ombi la utetezi.

**KESI YA KUJIBU**

Hakimu Mkazi Patricia Kisinda, anayesikiliza kesi hiyo, alisema baada ya mahakama kupitia vielelezo vya ushahidi na kuwasikiliza mashahidi 13 wa upande wa mashtaka, kuna kesi imejengeka, hivyo washtakiwa hao wana kesi ya kujibu.

Hakimu Kisinda alisema kutokana na kujengeka kwa kesi, baada ya kupitia ushahidi na vielelezo, washtakiwa hao watatakiwa kujitetea kwa mujibu wa sheria.

"Mahakama imepitia vielelezo vya ushahidi vilivyotolewa mahakamani na mashahidi kuthibitisha makosa yanayowakabili washtakiwa na wana kesi ya kujibu, hivyo watatakiwa kujitetea kwa mujibu wa sheria," alisema Hakimu Kisinda.

Baada ya kuzikiliza hoja za pande zote mbili, Hakimu Kisinda, aliahirisha shauri hilo hadi Januari 17, mwaka huu washtakiwa hao watakapoanza kujitetea mahakamani huko.

Upande wa Jamhuri katika kesi hiyo uliwakilishwa na Janeth Sekule, Tersila Gervas, Neema Mbwana na Richard Jakopio wakati upande wa utetezi uliwakilishwa na mawakili Mosses Mahuna, Edmund Ngemela na Fridolin Bwemelo.

**HABARI KITAIFA**

# Wakili adai namba ya mshitakiwa kesi ya Mbowe imeuzwa kwa mtu

**Na Kulwa Mzee**

WAKILI wa utetezi katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mallya, ameibua jambo mahakamani baada ya kudai kuwa laini ya simu ya mshtakiwa wa kwanza, Halfan Bwire, imeuzwa kwa mtu mwingine.

Mallya aliibua madai hayo jana katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi wakati akimhoji Mwanasheria wa Airtel, Gladys Fimbari, huku akidai kuwa namba hiyo aliyochunguza miamala, imeuzwa kwa mteja mwingine, Godson Munuo kwa Sh. 500.

Mallya alimbana maswali shahidi huyo mbele ya Jaji Joackim Tiganga wakati akitoa ushahidi kuhusu Luteni Dennis Urio mwenye namba 0787 555200 aliyetumiwa Sh 500,000 na Mbowe kwamba alitoa Sh. 300,000.

Alihoji kumbukumbu yoyote aliyotoa mahakamani kuonyesha Sh. 80,000 zilizotumwa kwa namba inayodaiwa ya Bwire zilikwenda wapi.

Akihojiwa shahidi alidai laini za Airtel wanauza kwa Sh. 500 na alipotakiwa kueleza kama anajua namba ya Bwire 0782 237913 kwa sasa imeuzwa kwa Godson Munuo kwa Sh 500, alidai hakujua kama imeuzwa.

Kuhusu fedha zilizokuwa katika namba hiyo ya simu, alidai zinawekwa katika akaunti ya kukusanya fedha.

Pia shahidi huyo alihojiwa na Wakili Peter Kibatala, anayeongoza jopo la kumtetea Mbowe na wenzake na kuulizwa kama anafahamu kuwa Mbowe ni Mwenyekiti wa CHADEMA na kwamba anashtakiwa kwa ugaidi.

Shahidi huyo alidai kuwa wanatakiwa kulinda haki za mteja na kwamba mteja kwao ni mtu muhimu, hivyo wanaangalia sana taarifa zake lakini pale panapohitajika kisheria wanafuata sheria kutoa taarifa hizo.

"Hakuna sheria inayokataza kuhoji amri ya kuwataka kutoa taarifa za mteja chombo kilichoomba taarifa za wateja kinaruhusiwa kisheria kupewa.

"Wakati natafuta taarifa za miamala kwa namba ya Mbowe, nilijua namba yake kwa sababu niliona aliyesaini (aliyetia saini) barua ya kuomba taarifa za namba za simu simjui. Barua ilikuwa na namba ya simu lakini sikuipiga isipokuwa baada ya wiki moja nilikwenda kutoa maelezo Polisi,"alidai shahidi.

Alidai kuwa barua iliyokwenda Airtel ilielekezwa kwa mwanasheria lakini hakuieleza mahakama barua hizo zinahifadhiwa wapi na wala hakusema polisi ilifikaje.

Fimbari alidai barua ya kuomba taarifa za miamala ilimfikia Julai 2, mwaka jana, na siku hiyo hiyo aliifanyia kazi na kujibu lakini hakusema kwa nini aliifanya kazi hiyo kwa haraka.

Alidai kuwa Airtel walikuwa hawafahamu kama Mbowe anashtakiwa kwa ugaidi kwa kuwa barua ilieleza taarifa hizo zinahitajika kwa ajili ya makosa ya jinai.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kuutambulisha mradi wa majaribio unaolenga kuzuia na kukabiliana na udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono. Kulia ni Mkaguzi Msaidizi wa Polisi Chritopher Newton. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Vigogo zaidi CCM wapigana vikumbo kuwania uspika wa Bunge la Tz

**Na Waandishi Wetu**

NI mwendo wa vikumbo. Ndivyo unavyoweza kusema kwa lugha nyepesi baada ya vigogo kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM) kupishana kwenda kuchukua fomu za kuomba kuteuliwa kugombea nafasi ya Spika wa Bunge la Tanzania.

Hadi jana jioni, idadi kamili ya makada wa CCM waliojitokeza kuchukua fomu hizo walikuwa 66, huku aliyekuwa Katibu wa Bunge, Dk. Thomas Kashililah tangu mwaka 2009 hadi 2017, akiwa miongoni mwa wanachama waliojitokeza.

Jana pekee, ni wanachama 17 waliojitokeza kuchukua fomu hizo akiwamo aliyekuwa Waziri wa Mifugo na Uvivi katika serikali iliyopita, Luhaga Mpina.

Katibu Msaidizi Mkuu, Idara ya Oganazesheni wa CCM, Solomon Itunda, akizungumza na waandishi wa habari jana katika ofisi za makao makuu ya chama hicho, jijini Dodoma, aliwataja mawaziri wengine wa serikali iliyopita waliochukua fomu ni aliyekuwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya na aliyekuwa Mbunge wa Ulanga, Goodluck Mlinga.

Alisema hadi juzi, wanachama waliochukua fomu walikuwa 49 na jana wakaongezeka 17, hivyo kufikia 66.

"Leo hii tumepokea wanachama 17 ambao wamejitokeza katika vituo vyetu vya Dodoma, Dar es Salaam na Ofisi Kuu ya Zanzibar kuchukua fomu za kuomba kuteuliwa kugombea nafasi hii ya Uspika iliyoachwa wazi," alisema Itunda.

Pia alisema katika kituo cha Dodoma, wanachama watatu walijitokeza kuchukua fomu na ofisi ndogo ya Lumumba walijitokeza 12 na Ofisi Kuu ya Kisiwandui, Zanzibar, wanachama wawili.

Itunda aliwataja waliochukua fomu Ofisi Kuu Dodoma kuwa ni Habibu Mgeja, Dk. Linda Salekwa Ole Saitabau, Norman Sigalla na Faraji Rushagama.

Alisema Ofisi Ndogo ya Lumumba, waliochukua fomu ni Emmanuel Sendama, Dk. Kashililah, Goodluck Mlinga, Bibie Mssumi, Hilal Hanin Seif, Athumani Mfutakamba, Mwenda Burton Mwenda, Henry Kessy, Josephat Malima, Adamu Mnyavanu, Stella Manyanya na Andrew Kevela.

Itunda alisema pia waliochukua fomu katika Afisi Kuu ya Zanzibar ni Luhaga Mpina na Hussein Migoda Mataka.


Aliwataka wanachama wa chama hicho kuitumia siku ya mwisho kujitokeza kuchukua fomu hizo, ili wapate haki yao ya kikatiba ya kugombea katika kinyanganyiro hicho.

Wakati huo huo, Mtaalamu mbobezi wa masuala ya kodi, Hamidu Chamani jana alirudisha fomu ya kugombea nafasi hiyo kwenye ofisi ndogo za chama Lumumba Jijini Dar es Salaam na kusema, anaamini anao uwezo wa kuongoza bunge na kukisaidia chama chake katika kuleta maendeleo ya nchi.

Chamani aliyewahi kuwania ubunge wa Kyerwa mkoani Kagera mwaka 2020 alisema idadi kubwa ya waliowania nafasi hiyo haimpi tabu kwa kuwa yeye ni bora zaidi yao.

Naye Ofisa Ardhi Mteule wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu mkoani Arusha, Wakili Faraji Rushagama, akichukua fomu alisema anatamani Spika ajaye asiwe mbunge ili Watanzania wapate ladha tofauti.

"Nimeamua kujitosa kumrithi aliyekuwa Spika wa Bunge, Job Ndugai, kwa sababu kiti hicho kiko wazi na katiba, inanipa fursa hiyo, kwa mujibu wa ibara ya 82. Spika si lazima awe mbunge, bali anaweza kuwa mwanachama wa chama chochote cha siasa," alisema Rushagama.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

Simu Nambari: +255(0)28 250 1044
Simu Nambari: +255 (0) 28 250 1045
Fax Na: 028 - 2500117
Unapojibu tafadhali taja:
Unapojibu tafadhali taja:

Ofisi ya Hakimu Mkazi Mfawidhi
Mahakama ya Mwanzo Mjini,
S.L.P. 155,
MWANZA.

Kumb. Na. MADAI 322/2021 11/1/2022


Afisa Masoko,
Ofisi ya Magazeti,
MWANZA

YAH: SHAURI LA TALAKA NA. 322/2021
MDAI:..........................................TUJIJENGE TANZANIA LTD
DHIDI YA
MDAIWA:.......................................... AMINA JOHN SABUHOLO

Unaamriwa na Mahakama ya Mwanzo Mjini Mwanza kufika tarehe 18/01/2022 saa 2.00 asubuhi bila kukosa ili kujibu madai yaliyofunguliwa hapa Mahakamani. Endapo hutafika Mahakamani shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi bila wewe kuwepo.

HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MWANZA.

HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MWANZA



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

Simu Nambari: +255(0)28 250 1044
Simu Nambari: +255 (0) 28 250 1045
Fax Na: 028 - 2500117
Unapojibu tafadhali taja:
Unapojibu tafadhali taja:

Ofisi ya Hakimu Mkazi Mfawidhi
Mahakama ya Mwanzo Mjini,
S.L.P. 155,
MWANZA.

Kumb. Na. MADAI 324/2021 11/1/2022

Afisa Masoko,
Ofisi ya Magazeti,
MWANZA

YAH: SHAURI LA TALAKA NA. 324/2021
MDAI:..........................................TUJIJENGE TANZANIA LTD
DHIDI YA
MDAIWA:.......................................... PATRICK JOHN MPUYA

Unaamriwa na Mahakama ya Mwanzo Mjini Mwanza kufika tarehe 16/02/2022 saa 2.00 asubuhi bila kukosa ili kujibu madai yaliyofunguliwa hapa Mahakamani. Endapo hutafika Mahakamani shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi bila wewe kuwepo.

HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MWANZA.

HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MWANZA

# Msimamizi fedha, biashara ataja sababu kujitosa uspika

**Na Gwamaka Alipipi**

MSIMAMIZI wa masuala ya fedha, biashara na uwekezaji, Dk. Godwin Maimu, amejitosa kuwania uteuzi wa nafasi ya Spika wa Bunge la Tanzania, kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), akisema anataka kwenda kuleta mabadiliko ya uongozi bungeni.

Dk. Maimu alifika ofisi ndogo za CCM Lumumba jijini Dar es Salaam majira ya saa 4:30 asubuhi na kuchukua fomu hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukabidhiwa fomu, Dk. Maimu alisema yeye ni kada wa muda mrefu wa CCM.

"Nampongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutaka kuwapo kwa mchakato wa kuwania nafasi hii. Mimi kama kijana nimejikagua nikaona ninatosha na ninafaa kuwania nafasi hiyo na ndiyo maana nimefika hapa leo," alisema Dk. Maimu.

Dk. Maimu alisema uchukuaji wa fomu ni hatua ya kwanza na kwamba Kamati Kuu ya CCM ikimpendekeza kuwania nafasi hiyo, ataitumikia kwa moyo wote na kwa maslahi mapana ya Taifa kwa sababu uwezo na nia anayo.

Alisema hatua ya kuchukua fomu siyo kwamba anakwenda kujaribu wala kutangaza jina lake, bali amekuwa na nia thabiti ya kushindana kupata nafasi hiyo na kwamba amekuwa akiwania nafasi mbalimbali ndani ya chama.

"Mwaka 2020 wakati wa uchaguzi mkuu niliwania nafasi ya ubunge Siha mkoani Kilimanjaro lakini kura hazikutosha. Nikashiriki katika mchakato wa kuinadi ilani ya chama na tukaibuka washindi," alisema Dk. Maimu na kuongeza;

Novemba, 2020 nilichukua fomu ya uteuzi wa nafasi ya Spika wa Bunge la Tanzania lakini jina langu halikufanikiwa kuteuliwa, Hivyo leo (juzi) nimekuja kuwania kwa mara ya pili. Nataka kuleta maendeleo chanya ndani ya CCM na Taifa," alisema.

Tangu kutangazwa kwa mchakato huo siku ya kwanza, wanachama tisa walijitokeza kuchukua fomu, siku ya pili walijitokeza wanachama nane na siku ya tatu wanachama 13.

Kwa mujibu wa CCM, Januari 17 mwaka huu, Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa itakutana kwa ajili ya kujadili wagombea na kuishauri Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa juu ya wagombea ambao wamejitokeza kuomba kiti hicho cha uspika.

Januari 18 hadi 19 mwaka huu, pia kutakuwa na kazi ya kuchuja na kufanya uteuzi wa mwisho ambapo Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ndiyo itafanya kazi hiyo.

Kadhalika, Januari 21 hadi 30 Kamati ya Wabunge wa CCM itapiga kura ya kumpata mgombea ambaye atakwenda bungeni kuomba kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge.

A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
KILIMANJARO DRINKING WATER

TAARIFA KWA UMMA

**BONITE BOTTLERS LTD** inapenda kuufahamisha umma juu ya kusitisha matumizi ya **plastiki laini (seal)** katika vifuniko vya chupa za **Maji ya Kilimanjaro** kutokana na agizo la serikali juu ya matumizi ya plastiki hizi kulinda mazingira.




@kilimanjaro_drinking_water kilimanjarodrinkingwater kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422

# CCM yatishia kuzifuta shule za Wazazi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimetishia kuzifuta shule za jumuiya za chama ambazo zimekuwa mzigo kwa kufanya vibaya kwenye matokeo ya mitihani ya mwisho.

Wakati tishio hilo likitolewa, kwa wakuu wa shule hizo wamepewa mwaka kuhakikisha wanabadilika.

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, alibainisha hayo jana jijini hapa wakati akizungumza kwenye mkutano wa wakuu wa shule na wahasibu wa shule za jumuiya hizo, kujadili kuhusu usimamizii wa shule, uendeshaji wake na usimamizi wa rasilimali na fedha.

Aliwataka wakuu wa shule hizo kujipima na kujitathmini ili kurudisha heshima ya shule hizo katika taaluma kwa lengo la kuondokana na matokeo mabovu.

"Nazifahamu vizuri shule za jumuiya ya wazazi licha ya kuwa na uwezo mzuri wa kufanya kazi kuna tatizo la kufanya vibaya. Sasa kuanzia mwakani, atakayefanya chini ya kiwango anatengeneza ziro au daraja la nne tutamnyang'anya apewe mwingine.

"Lazima tuvute soksi tukae sawa kwenye kila eneo maana hakuna miujuza ya kubadili 'perfomance'. Wekeni mipango yenye tija maana shule hizo hazifanyi vizuri kwa kila kitu na hata fedha inayopatika inafanyiwa ubadhirifu," alisema.

Chongolo alisema kwa sasa kuna mpango wa kuchukua shule ya Tabata ili kuiendeleza badala ya kuingia ubia na mtu mwingine kuonyesha mfano kama chama kwa kuhakikisha inakuwa na masomo ya kidato cha tano na cha sita.

"Tunaichukua kama chama ili tukikosea jumuiya ituulize hapa kimetokea nini na Mei 5, mwaka huu, tutaizindua na kuitangaza kama shule ya kidato cha tano na sita na tuweke wanafunzi ili nikija hapa niwe na nguvu ya kusema kuwa hapa mnatuangusha.

"Wakuu wa shule za jumuiya ya chama tuhakikishe tunaiga mfano wa shule zinazofanya vizuri nchini ili tujue ni kwa nini sisi hatufanyi vizuri na wapi panahitaji marekebisho,"alisema.

Kuhusu ubadhirifu unaofanywa kwenye fedha zinazotokana na shule hizo, Chongolo alisema fedha zinazopatikana si za mtu binafsi, hivyo lazima zitumike kwa utaratibu.

Chongolo alizitaka bodi za shule zifuatilie fedha hizo na ukaguzi kwa shule zisizowasilisha fedha ufanyike maana hakuna taarifa za shule zinazotuma fedha.

"Kuna kaugonjwa kakubwa tulipata wakati tunafanya ukaguzi maana hakuna taarifa za fedha maana hakuna shule zilizotuma taarifa za fedha, simamieni hilo maana na wewe(Mwenyekiti wa Jumuiya) unasimamiwa usikubali watu wakuangushe," alisema.

"Tumeni taarifa sahihi za fedha makao makuu ni lazima kuwepo mawasiliano ya moja kwa moja, wekeni utaratibu wa muda wa kuwasilisha kadri mtakavyokubaliana maana siko tayari kuona hilo linafanyika na tutafanya tathmini na tunatoa mwaka mmoja kwa shule mzigo kwenye chama kujitathimini," aliongeza.

## HABARI KITAIFA

# Ajeruhiwa vibaya kwa kugonga nyati

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

THOBIAS Mbilinyi (47), mkazi wa Makambako mkoani Njombe amejeruhiwa vibaya baada ya gari alilokuwa akisafiria kugonga wanyamapori wawili aina ya nyati waliofariki dunia papo hapo katika eneo la tukio, ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Mikumi, barabara kuu ya Morogoro-Iringa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Fotunatus Musilim, alithibitisha juzi kutokea kwa ajali hiyo ambapo Mbilinyi alijeruhiwa vibaya huku nyati wawili dume wakifariki dunia katika ajali iliyotokea Januari 10, majira ya saa 1:00 asubuhi.

Alisema ajali hiyo imehusisha gari dogo aina ya Toyota Crown lenye namba za usajili T 995 DLF lililokuwa likiendeshwa na Mbilinyi, likitokea Dar es Salaam kwenda Makambako na chanzo ni mwendo kasi wa dereva.

"Ndani ya hifadhi uendeshaji ni kilometa 70 kwa saa mchana na usiku ni kilometa 50 kwa saa, lakini dereva hakufuata taratibu na kusababisha ajali hii" alisema SACP Musilim.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Fotunatus Musilim.

Akabainisha kuwa majeruhi wa ajali hiyo alipelekwa kituo cha Afya Mikumi, baadaye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro alikopewa rufaa kwenda Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kutokana na majeraha makubwa aliyopata hasa sehemu za kichwa na shingoni.

Kamanda huyo wa Polisi alisema mtuhumiwa huyo akiruhusiwa kutoka hospitali anatarajiwa kufikishwa mahakamani kujibu mashtaka yanayomkabili.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Morogoro, Dk. Daniel Nkungu, alithibitisha kumpokea majeruhi huyo majira ya saa 5:00 asubuhi akitokea Mikumi na alikuwa ameumia sana maeneo ya usoni na shingoni. Alisema baada ya huduma ya kwanza ya dharura iliyochukua karibu muda wa saa moja, alisafirishwa kwenda Muhimbili.

Naye Kaimu Mhifadhi wa Hifadhi ya Taifa ya Mikumi, Herman Mtei, alisema nyati hao wawili waliogongwa, kila mmoja ana thamani ya Dola za Kimarekani 1,900 na kwamba mtuhumiwa atapewa adhabu mbalimbali kulingana na tukio hilo.

"Adhabu ambazo mtuhumiwa atalazimika kulipa ni pamoja na faini ya uchafuzi wa mazingira katika hifadhi ya Sh. 50,000, faini ya mwendokasi Sh. 50,000, faini ya kusababisha ajali hifadhini Sh. 200,000 na faini ya kugonga nyati kila mmoja atalazimika kulipa Dola za Kimarekani 1,900,"alisema Mtei.

Hifadhi ya Mikumi inakatizwa na barabara kuu ya Morogoro-Iringa, jambo linalosababisha vifo kwa wanyama, uchafuzi wa mazingira na wapita njia kubadilisha tabia za wanyama kwa kuwalisha wanyama vyakula vinavyotumiwa kibinadamu na utalii wa bure kwa wapita njia.

Hata hivyo Serikali kwa kuliona hilo ilianza mchakato wa ujenzi wa kiwango cha lami kwa barabara ya Turiani-Magole-Dumila-Rudewa-Kilosa hadi Mikumi ili pamoja na mambo mengine, iondoe ulazima uliopo sasa wa watumiaji wa magari kukatiza bure ndani ya hifadhi hiyo.


### TANGAZO LA NOTISI - WADAIWA SUGU

**TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICE LIMITED,** Inatangaza notisi ya siku Sitini (60) Kuanzia tarehe ya Tangazo hili. Hatua zaidi za Kisheria zitachukuliwa kwa wadaiwa watakaoshindwa kulipa madeni yao ndani ya muda ulioainishwa( siku sitini).Ikiwa ni pamoja na kuwaruhusu madalali kuuza mali zao ambazo zimewekwa dhamana za mikopo yao.

**Wadiwa Sugu ni:**

1. Sarafina Rafael Msengi- Rada chuo- Majohe (DSM)
2. Faisal Said Muhamed - Rada chuo- Majohe (DSM)
3. Ally Mohamedi Matika – Nzasa 'A' Kilungure (DSM)
4. Mariam Emilian John-Pugu bombani (DSM)
5. Fadhili Abdurahman Mpinga –Majimatitu 'A' Mbagala (DSM)
6. Salma Mohamed – Kwembe,Ubungo (DSM)
7. Rehema Makau – Bonyokwa Kisiwani (DSM)
8. Flora Nyamhanga-Mwanadilatu (Mkuranga)
9. Faustine Mabagala Thumuni- Nyamanoro Mashariki (Mwanza)
10. Regina Albert Vakolavene- Msingwa (DSM)
11. Bahati Kapili Lwama- Luchelele (Mwanza)
12. Prisca Revocatus Mgeta –Lwanhima( Kishiri) Mwanza
13. Waven Esrom Mrikalia(Mdhamini)-Ndope Kishiri/Marco Esrom Mrikalia(Mkopaji) – Mabatini Mwanza

**Mawasiliano piga:**
+255 222774742-3/0718068335/0718730242
Au Email: tujijengetanzania@tujijenge.or.tz



## NOTISI/TANGAZO

MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, NGOMENI AUCTION MART,MOPEH COMPANY LTD,KOTI BROTHERS LTD,MBUZAX AUCTION MART kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| TANDALE | ZAITUNI OMARY JUMA | NYUMBA | ZAITUNI OMARY JUMA | KIVULE | 31/01/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | GILASIO DANIEL SOKA | NYUMBA | ASNATI ATHUMAN RAJABU | MSAKUZI | 31/01/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | BENJAMIN PATRICK MABINZA | NYUMBA | BENJAMIN PATRICK MABINZA | MBEZI MSAKUZI | 2/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | ATHUMANI HASSANI HEMEDI | NYUMBA | ATHUMANI HASSANI HEMEDI | ULONGONI 'B' | 16/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA (2) | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | MBEYA MJINI NA TUNDUMA | 10/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | MATHIAS EUSEBIO MBONDE | NYUMBA | MATHIAS EUSEBIO MBONDE | KIMARA STOP OVER | 9/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | TIMOTHY LUCAS MANYAMA | NYUMBA | TIMOTHY LUCAS MANYAMA | MIEMBE SABA KONGOWE | 3/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KINONDONI | ALEX NAHUMU PALANGYO | NYUMBA | JOSEPH BENJAMIN | MBEZI MTONI | 4/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | GREEN RIVER LIMITED | NYUMBA | LAFAEL ISMAIL HUZILWA | BUNJU 'B' | 8/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | RICHARD DANIEL MOSHI | NYUMBA | VIVIAN HENRY MSACKY | KIKARARA | 9/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | DANIEL ELISAMIA KIMARO | NYUMBA | DANIEL ELISAMIA KIMARO | BONITE | 31/01/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | KISAMO BROTHERS | NYUMBA | JAPHET ALLEN MERO | MAJENGO | 3/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | NEEMA SOLOMON MWANGA | NYUMBA | NEEMA SOLOMONI MWANGA | BOMA | 4/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | ALEX SABAS SILAYO | NYUMBA | ALEX SABAS SILAYO | CHEKERENI | 8/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | JAMES PATRICK MUSHI | NYUMBA | JAMES PATRICK MUSHI | OLERIEN MUSHONO | 29/01/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | SIRILI PANTALEO MATERU | NYUMBA | SIRILI PANTALEO MATERU | NJIRO-ARUSHA | 2/02/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | GALVAS NDALUKA MAZURI | BAJAJI (2) NAMBA MC215CAW NA MC 702CCM | GALVAS NDALUKA MAZURI | MWANZA MJINI | 31/01/2022 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | JOSEPH KIGONGO IBAMBASI | NYUMBA | JOSEPH KIGONGO IBAMBASI | NYAKATO | 29/01/2022 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

MASHARTI YA MNADA

| | |
|---|---|
| 1 | Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba au Kiwanja ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14. |
| 2 | Ikiwamnunuziatashindwakutimizashartilolote la mnada kuhusiana na malipo yaawali,hatarudishiwapesayoyotealiyokwishailipa. |
| 3 | Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0715363537/0714939933/0715467455/0621800779/0710885084 |
| 4 | Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote. |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Dirisha dogo la usajili liwe la kujenga si kukomoana

**USAJILI** wa dirisha dogo kwa ajili ya wachezaji wanaoshiriki Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, Ligi ya Championship (zamani Ligi Daraja la Kwanza), First League (Ligi Daraja la Pili) na Ligi Kuu ya Wanawake nchini linatarajiwa kufungwa leo saa 5:59 usiku.

Lengo la dirisha hili dogo la usajili ni klabu kupata nafasi ya kurekebisha na kuimarisha vikosi vyake kutokana na mapungufu waliyoyabaini katika mechi ambazo wameshacheza katika ligi husika wanazoshiriki, mashindano ya kimataifa na michuano ya Kombe la FA.

Klabu itakayotumia vyema dirisha hili dogo la usajili, hakika matunda yake yataonekana ndani ya muda mfupi na si vinginevyo.

Timu zitakazowaachia makocha wao kufanya mchakato wa safu ipi inahitaji kuboresha, hakika itakuwa kwenye nafasi nzuri ya kupata matokeo chanya baada ya kusajili wachezaji wapya katika dirisha hili lililofunguliwa tangu Desemba 15, mwaka jana.

Kama ambavyo timu husika inafahamu mahitaji yake halisi, na ikayatendea haki, ni ukweli usiofichika timu hiyo itarejea katika hatua ya mwisho ya lala salama ya msimu ikiwa imara na ikielekea kwenye kutimiza ndoto na malengo yake iliyojiwekea katika msimu huu wa mwaka 2021/22.

Timu inaweza ikakumbana na changamoto ya fedha katika kukamilisha usajili wake, lakini bado inatakiwa kuwa na suluhisho au machaguo yanayozidi mawili ili kufanikisha lile ambalo inalihitaji kwa ajili ya kuboresha kikosi chake ambacho kiko kwenye mbio za ubingwa au kujinusuru na kushuka daraja. Lakini katika hali isiyo ya kawaida, kuna klabu zinaendelea na mchakato huu bila kuhusisha makocha wake ambao kwa taaluma yao wanajua mahitaji halisi ya timu yao na wanachohitaji ili kufikia malengo ya kucheza soka la ushindani wakati wote.

Itashangaza kuona katika dunia ya sasa bado viongozi wa timu za hapa nchini wanasajili wachezaji wapya kwa shinikizo kutoka upande fulani au kumkomoa mpinzani wako. Ieleweke kufanya hivyo si tu kuiumiza timu yao, lakini pia ni kukiweka mashakani kipaji cha mchezaji husika.

Kusajili mchezaji ambaye hayuko katika mipango ya kocha ni jambo ambalo linarudisha nyuma maendeleo ya timu au ligi kwa ujumla, lakini pia inapoteza nafasi ya mchezaji kuendeleza kipaji chake. Ili kuachana na 'mauzauza' haya, umefika wakati makocha wakapewa nguvu na viongozi wakabakia na nafasi yao ya kukamilisha taratibu za kiutawala.

Mpaka sasa kwenye ligi zote zinazochezwa hapa nchini hakuna timu ambayo iko salama katika mbio za ubingwa au kwa wale wanaoburuza mkia kusema ni lazima watashuka daraja. Muda wa kufanya marekebisho kwa weledi bado upo na saa chache zilizobakia zinaweza kubadilisha mwelekeo wa timu husika.

Kikubwa ili kufikia malengo, viongozi wanatakiwa kuwapa makocha nafasi ya kukamilisha mchakato huu kikamilifu na hapo baadaye timu itakapofanya vibaya, watawajibika kutoa maelezo huku hatua nyingine zinaweza kuchukuliwa kulingana na makubaliano wakati wanakabidhiwa mikoba ya kufundisha timu hizo.

Tunawakumbusha ligi zote bado ni changa na mpaka sasa hakuna klabu ambayo iko salama kwenye kufikisha malengo yake ndani ya msimu huu. Lolote linaweza kutokea na kubadilisha msimamo uliopo sasa na kuwashangaza wote ambao waliamini msimu huu kwao unaweza kuwa wa furaha. Ni jambo la kushangaza baadhi ya timu zinaanza kurudi kule ambako tulishakusahau kwa kugombea mchezaji ambaye kwa 'macho' ya nje tayari alishafanya mazungumzo na timu nyingine, hili linaweza kuwa na faida endapo nyota huyo atafanya vyema, lakini itaonekana 'mkosi' endapo mchezaji huyo husika atashindwa kuonyesha kiwango bora baada ya kusajiliwa.

Jambo la msingi na la kuzingatiwa kwa maendeleo ya soka hapa nchini kwenda kwa wahusika wote ni kufahamu dirisha dogo la usajili linatakiwa kutumiwa kwa maana halisi iliyowekwa na kamwe isiwe kwa 'kukomoana' kwa sababu kwa kufanya hivyo, klabu husika haitafaidika lakini pia nafasi ya kuendeleza timu au maslahi ya mchezaji huenda yakawa shakani.

Kwa maendeleo ya timu, ni vyema kutumia saa chache zilizobakia kabla ya dirisha la usajili halijafungwa, kukamilisha michakato itakayojenga na si vinginevyo maana hakuna mechi rahisi msimu huu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Waamuzi Bongo walindeni wachezaji

Na Adam Fungamwango

**KWA** siku za karibuni kumeonekana kuna aina fulani ya uchezaji wa kihuni katika soka la Tanzania ambao unaonekana kama unaanza kuhalalishwa na baadhi ya waamuzi.

Soka hili baadhi yetu tulikuwa tukiliona miaka ya nyuma kwenye miaka ya 1980, mabeki walipokuwa wakicheza kikatili, makipa wakiruka na miguu, lakini pia kulikuwa na uhuni mwingine kwenye mchezo wa soka ambao ulisababisha hata baadhi ya wazazi kuwakataza watoto wao kuingia katika mchezo huo.

Ulionekana kama vile ni mchezo wa watu wenye nguvu kama vile raga, lakini rafu zilikithiri na sheria hazikuwa ngumu sana kwa wachezaji kiasi kwamba ili kucheza soka ni lazima uwe mbabe hivi.

Baada ya soka kugeuka sasa kuwa biashara, makampuni yakawekeza fedha nyingi, Shirikisho la Soka Duniani (FIFA) lilibadilisha sheria nyingi na kuuweka mchezo huo kuwa na burudani zaidi badala ya ubabe na uhuni.

Zamani beki alikuwa na uwezo wa kukurukia miguu miwili sehemu yoyote ya mwili, na labda ikatoka kadi ya njano tu, kipa aliruka na silaha ambayo ni mguu kuweka mbele, kwa sababu tu yeye mwenyewe hakuwa analindwa, kwani hata akiguswa na kusukumwa kwa kutumia mwili wa mchezaji mwingine haikuhesabika ni faulo.

Ndiyo maana kwenye kona, kuna mchezaji kazi yake ilikuwa ni kumsukuma kipa na mmoja kupiga kichwa.

Lakini huyo atakayekwenda kumsukuma kipa ni lazima awe mbabe kweli kweli kwa sababu makipa wenyewe wa zamani walikuwa ni wababe, na watukutu na si rahisi sana kufanya hivyo.

Mabeki waliwachezea mastraika rafu za hovyo, ndiyo maana kwanza kabisa ikawekwa sheria kuwa akiwa mtu wa mwisho akicheza rafu ni kadi nyekundu, na mchezaji yoyote atakayemkwatua mwenzake kwa nyuma, wakati tayari ameshapitwa ni kadi nyekundu pia. FIFA walitengeneza sheria kuwa rafu zitakazoachwa ni zile za kimpira, lakini yoyote ile inayoonekana kuhatarisha maisha ya mchezaji mwenzake, au 'karia' yake ya kucheza soka moja kwa moja ni kadi nyekundu.

Kwenye Ligi mbalimbali za Ulaya na hata baadhi ya nchi za Afrika, ikiwamo hata katika Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho, waamuzi wamejitahidi sana kuzingatia hilo.

Cha ajabu hapa nchini, waamuzi wamekuwa bado wanachezesha soka la miaka ya 1970 hadi 1980. Katika Ligi Kuu Tanzania Bara na hata Kombe la Mapinduzi tumeona baadhi ya rafu mbaya, za kihuni ambazo waamuzi wameonekana kuogopa kutolea uamuzi.

Ifike wakati waamuzi wa Tanzania waache wachezaji wanaotaka kucheza soka, kuonyesha ufundi na burudani kwa mashabiki wapewe uhuru wa kufanya hivyo na ambao wanaona soka ni mchezo wa kihuni, kazi yao ni kutaka kuumiza wengine wapewe adhabu ya kutolewa nje.

Sikatai kuwa soka linahitaji nguvu na kupambana, hiyo inaeleweka, lakini yoyote anayependa soka na aliyecheza anajua jinsi gani ya kutumia nguvu kwenye soka na kucheza rafu ya kuhatarisha maisha ya mchezaji mwenzako. Waamuzi wa Ulaya hawa huwa hawakopeshi, rafu moja tu ya kutaka kumuumiza mwenzako ni kadi nyekundu moja kwa moja.

Hapa nchini waamuzi wamewafanya wachezaji kama ng'ombe, na kuacha wachezewe rafu za kikatili na kutisha, huku wakitoa kadi chache za njano kwa sababu ya kinachoonekana woga tu.

Mchezaji mwenye uwezo anatakiwa kunyanga'anywa mpira na mchezaji mwenye uwezo pia. Kwa sababu yeye ni mchezaji, anatakiwa pia atumie uwezo wake na nguvu zinazoruhusiwa kwenye soka na si rafu za kupigana miguu ya tumbo, kichwani, mbavuni kama wacheza karate na kung'fu, huku kukiwa hakuna uamuzi wa maana ya kuwaadhibu unaofanyika.

Kama waamuzi wataendelea kulea aina hii ya uchezaji wa kihuni wa baadhi ya wachezaji ulioanza kuzoeleka, kuna uwezekano ipo siku tutapoteza wachezaji kwa kupata vilema vya maisha au kupoteza maisha kwa sababu tu ya udhaifu wa waamuzi kuchukua hatua. Mwamuzi anapochukua hatua, wachezaji huogopa kufanya hivyo kwa kuhofia kupewa kadi nyekundu, lakini anapoachia, basi anawapa uhuru kufanya wanavyotaka.

# Wanafunzi afya waonywa udanganyifu wa mitihani

**Na Neema Hussein,** MPANDA

WANAFUNZI wa Chuo cha Afya Mpanda mkoani Katavi, wametakiwa kuwa waaminifu na kuepuka udanganyifu katika masomo hasa kipindi cha mitihani kwa kuwa fani wanazosomea ni nyeti kwa maisha ya binadamu.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, alisema hayo jana wakati akizungumza na wanafunzi na watumishi wa chuo hicho baada ya kukabidhiwa madarasa yaliyojengwa kwa ufadhili wa Christian Social Services Commission (CSSC).

Mrindoko aliipongeza Wizara ya Afya kwa kuhakikisha chuo hicho kinafanya kazi kwa mara nyingine ikiwa ni baada ya kufungwa kwa miaka mingi.

"Nichukue nafasi hii kuwaomba Wizara ya Afya kuendelea kukisimamia chuo hiki tukishirikiana na sisi watumishi wa mkoa kuhakikisha watumishi wanapatikana kwa idadi inayotakiwa ili masomo yatolewe vizuri," alisema Mrindoko.

Mkuu wa Chuo hicho, Lightness Michael, alisema chuo kinakabiliwa na upungufu wa walimu, vitabu vya kufundishia, madarasa na ofisi za walimu. Alisema kwa sasa chuo kina walimu 10 na wanafunzi 119 huku walimu hao wakiwa saba wa kudumu na watatu wa muda.

"Chuo hiki kilianza mwaka 1974 kikasimama mwaka 1996. Baada ya hapo kwa juhudi ya Wizara ya Afya na ofisi yako, kikaanza tena mwaka mwaka 2020 kwa kuanza na wanafunzi 50," alisema.

Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Mpanda, Eusebius Nzigirwa, aliyeiwakilisha CSSC, alisema wanatoa huduma za kijamii ambazo ni wito uliotoka kwa Mungu wa kumhudumia mwanadamu kiroho, kimwili na kiakili.

"Sisi tumekuja kuwakilisha wenzetu kukabidhi darasa jipya na maabara iliyokarabatiwa kwa marafiki na wadau wa CSSC. Sisi tunafanya huduma zetu na tunahitaji msaada wa serikali na muda wote tumekuwa tukifanya nao kazi na ni wadau wakubwa wa serikali," alisema.

Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Magharibi, Sospeter Magesse, alisema wamekabidhi meza 100 na viti 100 vyenye thamani ya Sh. milioni 10 ambavyo vitatumiwa na wanafunzi kwenye darasa lililojengwa.

"Benki yetu imeendelea kuyafanya haya na si mara ya kwanza. Benki yetu imekuwa ikitenga asilimia moja kila mwaka kuipeleka kwenye sekta za afya na elimu kwa sababu tunajua tukiwa na taifa lenye afya, tutafanya maendeleo na tukiwa na watu wenye elimu, tutafanya maendeleo. Kwa hiyo afya na elimu ni sekta za kipaumbele," alisema Magesse.

# Msako mkali waliochepusha maji

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI wilayani Morogoro imeziagiza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MOROWASA) na Bonde la Wami/Ruvu kufanya operesheni maalumu kuwasaka watu waliochepusha maji katika mito inayoingiza maji katika Bwawa la Mindu.

Watu wamechepusha maji katika vyanzo vya mito hiyo kwa ajili ya shughuli za kibinadamu, hivyo kusababisha upungufu wa maji katika bwawa hilo. Mito hiyo ni Mzinga, Ngerengere, Mgeta na Mlali.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando, alitoa agizo hilo jana baada ya kufanya ziara ya siku mbili katika mito na vyanzo vya maji na kushuhudia baadhi ya watu wakiwa wamechepusha maji kwenye mito hiyo kwa ajili ya shughuli za kilimo.

"Agizo la serikali nendeni mkafanye operesheni ya kuondoa watu waliochepusha maji kwenye mito yote ambayo ni chanzo cha maji katika Bwawa la Mindu.

Asije kutokea mtu anasema eti kumwagilia shamba au nyanya ni bora, kafanyeni shughuli kuokoa wana Morogoro. Sheria ipo kamateni, pelekeni Mahakamani mara moja," alisema Msando.

Mkuu huyo wa wilaya alisema wakazi wa Manispaa ya Morogoro wanalitegemea Bwawa la Mindu kwa asilimia 70 kwa ajili ya kupata maji, hivyo uharibifu unaofanyika wa kuchepusha maji endapo utachwa, kuna hatari siku zijazo wananchi hao wakakosa maji.


Msando alisema pamoja na kuwapo kwa ukame katika kipindi hiki, mvua zinapoanza kunyesha ni lazima sasa kila nyumba ipande miti miwili pamoja na wananchi kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali kupanda miti katika maeneo ya vyanzo vya maji.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Morowasa, Mhandisi Tamimu Katakweba, alisema uharibifu wa mazingira, kuingiza mifugo na uchepushaji wa maji katika vyanzo vya maji ni moja ya sababu za kukauka kwa mito ambayo ndiyo tegemeo la kuingiza maji katika Bwawa la Mindu.

Alisema kwa sasa MOROWASA inatekeleza miradi mikubwa yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 13 pamoja na kujenga miundombinu mbalimbali ya kusambaza maji katika Manispaa ya Morogoro.

Katakweba alisema endapo uharibifu wa mito hiyo utaendelea, miradi hiyo itakuwa haina maana yoyote na wakazi hao wataendelea kukosa huduma ya maji.

Mhandisi wa Rasilimali za Maji kutoka Bonde la Wami/Ruvu, John Kassambili, alisema wataanza mara moja operesheni hiyo kuwakamata wale wote waliochepusha maji katika mito yote katika mkoa wa Morogoro na kuwataka wananchi kuwapa taarifa kwa watu wanaofanya hivyo.




Mkuu wa Huduma za Kifedha wa Tigo Pesa, Angelica Pesha akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni moja kwa Mkazi wa Gongo la Mboto, Yusuph Nehemia baada ya kuibuka mmoja wa washindi 10 wa Sh. milioni moja kila mmoja katika promosheni ya mwisho wa mwaka 2021 ya "Lipa kwa Simu Uwini", jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watalii wazidi kumiminika Kazimzumbwi

**Na Joseph Mwendapole**

IDADI ya watalii wanaotembelea Hifadhi ya Msitu wa Kazimzumbwi Pugu Mkoa wa Pwani imeongezeka na kufikia 10,206 mwaka huu.

Hayo yalibainishwa na Kamanda wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Kanda ya Mashariki, Caoroline Malundo, wakati wa ziara ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Seleman Jafo hivi karibuni.

Waziri Jafo alikuwa kwenye ziara ya siku moja kwa ajili ya kuangalia utunzaji wa mazingira akiambatana na viongozi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Alisema mwaka 2016/17 kulikuwa na watalii 533, mwaka uliofuata watalii 805, mwaka mwingine watalii 1,735, mwaka 2020/2021 watalii 8,732 wakati mwaka 2021/22 watalii walifikia NI 10,206.

Malundo alisema hali ya hifadhi kwa sasa inazidi kuimarika kutokana na jitihada mbalimbali za uhifadhi zinazofanywa na TFS kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, jamii zinazopakana na hifadhi na wadau mbalimbali wa uhifadhi. Alisema kutokana na kuimarika kwa uhifadhi, huduma mbalimbali za kijamii na za kiikolojia zikiwemo hewa safi, vyanzo vya maji, ufugaji nyuki, matambiko na utafiti wa kisayansi vinapatikana kupitia hifadhi hiyo.

mwaka wa fedha wa 2020/21, alisema walipanda miti 38,520 kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa mazingira wakiwamo WWF, Mpingo Foundation, DAWASA, Kimani na Shule ya Sekondari Minaki.

Kamishna huyo alitaja changamoto zinazowakabili kuwa ni uchimbaji wa udongo ndani ya hifadhi maeneo ya Pugu Mnadani, ukataji wa miti kwa ajili ya kujenga nguzo na uvamizi kwa ajili ya makazi na kilimo hasa safu ya Kazimzumbwi.

# Maofisa, askari TFS wapata mafunzo ya usalama baharini

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

MAOFISA na Askari 40 kutoka Jeshi la Uhifadhi la Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), wamepatiwa mafunzo ya usalama baharini katika chuo cha Wakala wa Elimu na Uvuvi, Mbegani, Bagamoyo mkoani Pwani.

Akifungua mafunzo hayo jana, Kamanda wa Kanda ya Mashariki, Kamishna Msaidizi Caroline Malundo, alisema mafunzo hayo yanalenga kutoa elimu ya usalama binafsi wakati wa utekelezaji wa shughuli za mikoko, uokoaji wa binadamu inapotokea dharura wakati wa doria za baharini.

Hotuba ya Kamishna wa Uhifadhi wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo ambayo iliwasilishwa na Kamishna Msaidizi Malundo, ilisema mafunzo hayo yatakuwa msaada katika kutekeleza shughuli za uhifadhi upande wa mwambao wa bahari hususani kuzuia uhalifu na uharibifu wa rasilimali za mikoko

Alisema mafunzo hayo yanafanyika ikiwa ni utekelezaji wa mpango mkakati wa TFS wa mwaka 2020- 2025 wa kuwajengea uwezo watumishi wa TFS wanaofanya kazi katika mazingira ya pwani ya bahari.

Maofisa watano na askari 16 wanaelezwa kunufaika na mafunzo hayo kwa mwaka 2020/2021 ambapo mwaka 2021/2022 maofisa 13 na askari 27 wanapatiwa mafunzo hayo.

Malundo alisema taasisi hiyo itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi kadri inavyowezekana na kuhakikisha rasilimali za mikoko zinalindwa.

Awali, Malundo alisema watumishi wa taasisi hiyo walikuwa na upungufu wa uelewa wa mbinu za kuchukua tahadhari wanapokuwa baharini wakitekeleza majukumu yao.

"Baada ya kuingia jeshi tumeona tuna umuhimu kwa watumishi wanaoshughulika na mikoko kupatiwa mafunzo haya ili wawe imara na kutekeleza majukumu yao wakiwa hawana wasiwasi mafunzo haya yatakuwa endelevu," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA), Makamu Mkuu wa Chuo, Eileen Nkondola, aliihakikishia TFS kwamba malengo ya askari na maofisa hao kupatiwa mafunzo, yatatimia kwa kuwa wamejipanga kwa kazi hiyo.

Washiriki wa mafunzo hayo ni kutoka mikoa ya Dar es Salam, Pwani, Lindi, Mtwara na Tanga.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema (kushoto), akikabidhi msaada wa pikipiki aina ya SanLG yenye namba za usajili MC 110 DCP yenye thamani ya Sh. milioni 2.4 kwa Darlen Athanasi mkazi wa Segese Msalala, wilayani Kahama, jana, kwa ajili ya kufanya shughuli za bodaboda ili kumuingizia kipato. Kushoto ni Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, George Kyando. **PICHA: MARCO MADUHU**

# RC amkabidhi mwanamke zawadi bodaboda

**Na Marco Maduhu**, KAHAMA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, amemkabidhi msaada wa pikipiki Darlen Athanasi (27), mkazi wa Segese wilayani Kahama, kwa ajili ya kufanya shughuli za bodaboda ili kumwingizia kipato.

Mjema alimkabidhi jana mwanamke huyo pikipiki hiyo yenye thamani ya Sh. milioni 2.4 ikiwa ni ahadi yake ambayo aliombwa kwenye mkutano wa hadhara, uliofanyika Segese mwaka jana.

Alisema alifarijika kwa ujasiri aliouonyesha mwanamke huyo wa kuamua kufanya shughuli za bodaboda, kwa ajili ya kujipatia kipato na kuendesha maisha yake kwa kutumia pikipiki ya kukodi, ndipo akaona ni vyema ampatie pikipiki yake mwenyewe.

"Namkabidhi pikipiki mwanamke huyu ambayo ataitumia katika shughuli zake za bodaboda na kuendesha maisha yake. Ni mwanamke jasiri sana ambaye habagui kazi na nimetimiza ahadi yangu ambayo aliniomba kwenye mkutano wa hadhara," alisema Mjema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, George Kyando, alimtaka mwanamke huyo akapitie mafunzo ya udereva na kumwahidi kumkatia leseni bure ili ajue sheria za usalama barabarani na kujiepusha na ajali.

Pia alimtaka akawe balozi mzuri wa kupinga matukio ya uhalifu pamoja na kutoa taarifa za wahalifu, akibainisha kuwa bodaboda huwa wanakutana na watu wengi, jambo ambalo litasaidia kukomesha uhalifu mkoani hapa.

Darlen alimshukuru mkuu huyo wa mkoa kwa kumpatia pikipiki hiyo akisema itamsaidia kuendesha familia yake kwa kuwa anaishi na watoto wake wawili na mama yake mzazi.

# Wahandisi wanawake watakiwa kusajiliwa ERB ili kutambulika

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), imewataka wanafunzi wote wa kike kutoka vyuo mbalimbali wanaosomea fani za ujenzi kujisajili katika Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) ili kuingia katika mfumo maalumu wa kihandisi.

Mhandisi Nancy Mduma kutoka ERB, alisema hayo jana wakati akifungua semina elekezi kwa wanafunzi wa kike kutoka Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia (MUST), kwenye ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara.

Mduma alisema kuna umuhimu mkubwa kwa wahandisi wanaomaliza vyuo kujisajili katika bodi hiyo kwa kuwa kuna kazi zingine za kihandisi zinataka mtu aliyesajiliwa tu.

"Serikali sasa inalenga kuwawezesha wahandisi wanawake kufikia madaraja ya juu ya uhandisi. Ili kufikia madaraja hayo ni bora kila mhandisi baada ya kumaliza chuo ajisajili na kuingia kwenye mfumo wa ERB, " alisisitiza Mduma.

Mratibu kutoka CRB, Mhandisi Victoria Haule alisema kazi kubwa ni kuwahamasisha wanawake kushiriki katika kazi za barabara ili kuongeza wigo mkubwa wa maendeleo unaofanywa na wanawake kutoka sehemu mbalimbali.

Mada zingine zilizotolewa ni pamoja na kuangalia mchakato wa usajili kwa kampuni za wanawake na kupitia mwongozo wa kuimarisha ushiriki wa wanawake katika kazi za barabara na masuala mtambuka.

Zaidi ya wanachuo 70 wameshiriki katika uwasilishwaji wa mada mbalimbali zinazohusu kushiriki kazi za barabara.



## Chanzo migogoro ya wanyama, watu chawekwa bayana

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ONGEZEKO la idadi ya watu nchini na mahitaji ya ukuaji imechangia kwa kiasi kikubwa migogoro kati ya binadamu na wanyamapori kutokana na kugombea maliasili zilizopo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Dk. Cecilia Leweli kutoka Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI) migogogoro kati ya binadamu na wanyamapori imesababisha hasara kubwa za kijamii, kiuchumi na

kibioanuwai pamoja na uhifadhi wa wanyamapori.

Alisema kuingiliwa kwa makazi ya wanyamapori pamoja na shoroba kunatishia uhusiano wa kiikolojia wa maeneo yaliyohifadhiwa.

"Migogoro kati ya binadamu na wanyamapori inatishia sana usalama wa makazi ya wanyamapori," alisema Dk Leweri.

Alisema ushahidi wa kiutafiti unaonyesha kwamba kuna shoroba za wanyamapori ambazo katika ardhi za vijiji zinatumika kwa shughuli mbalimbali zikiwamo za makazi, kilimo na ufugaji.

"Ni dhahiri kuwa kukithiri kwa migogoro hii kunachangiwa kwa kiasi kikubwa na hali ya umaskini, ukosefu wa teknolojia na utekelezaji duni wa malengo ya kisekta.

Dk. Leweri alisema mapitio ya utafiti mbalimbali yanapendekeza kwamba ili kukabiliana na migogoro hiyo, kwanza ni lazima sera zote zinazohusiana na matumizi ya ardhi ziunganishwe kuhusu masuala yote ya matumizi ya ardhi.

Alisema mabadiliko chanya katika mtazamo wa jamii kuhusu uhifadhi wa wanyamapori katika maeneo mengi na kuimarishwa kwa shuhuli za uhifadhi nchini vimesababisha wanyamapori wengi kuwa huru na kuingia katika makazi ya watu, hivyo kusababisha uharibifu.

Mtaalamu huyo alisema kuwa ongezeko la wanyamapori si kubwa kiasi cha kusababisha madhara kwa watu na mali zao ikilinganishwa na miaka ya 1970 hadi 1990 ambapo idadi ya watu ilikuwa takribani million 30, huku idadi ya wanyamapori mfano tembo ikiwa 300,000.

Alisema wakati mwaka 2020 idadi ya watu ni milioni 60 idadi ya tembo ni takribani 60,000 na kubainisha kwamba ongezeko la tembo ni dogo ikilinganishwa na idadi ya watu.

Dk Leweri alisema ongezeko hilo limechangia kwa kiasi kikubwa kupanuka kwa miji na shughuli mbalimbali za kijamii kwa mfano kilimo na ufugaji zinazomwingizia mwanadamu kipato.

# Waziri apiga marafuku michango shuleni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, amesema ni marufuku mwanafunzi wa elimu ya awali, darasa la kwanza au kidato cha kwanza kutozwa mchango wowote kama sharti la kuandikishwa.

Bashungwa alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizindua kalenda ya utekelezaji wa mitaala na mafunzo kwa maofisa elimu wa mikoa na wadhibiti wakuu wa ubora wa shule kanda.

Alisema shule za msingi na sekondari zinatarajiwa kufunguliwa Januri 17, mwaka huu, na kumeanza kujitokeza malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu kutozwa michango mbalimbali bila kufuata utaratibu.

Bashungwa alisema changamoto hizo zimekuwa zikisababisha usumbufu kwa wazazi na wanafunzi na kwa wananchi kwa ujumla.

"Vikwazo na kero hizi zimefifisha kwa kiasi kikubwa uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza na elimu ya awali.

"Nachukua nafasi hii kuwaelekeza viongozi wa mikoa, halmashauri na shule kuhakikisha hakuna mwanafunzi wa elimu ya awali, darasa la kwanza au kidato cha kwanza anayetozwa mchango wowote kama sharti la kuandikishwa," alisema.

Pia aliagiza kila shule kuwapo mwalimu angalau mmoja kwa ajili ya kuandikisha watoto katika kipindi hiki ambacho wanafunzi wako likizo.

Alisema viongozi wote wa TAMISEMI wahakikishe wanasimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Utoaji wa Elimu Msingi Bila Malipo.

"Mheshimiwa Rais ameongeza fedha zinazotolewa kila mwezi kwa ajili ya kugharimia elimu bila malipo kutoka Sh. bilioni 23 kwa mwezi hadi bilioni 26" alisema.

Pia alisema maofisa elimu wa kata kwa kushirikiana na watendaji wa kata, mitaa na vijiji, wabainishe watoto wote wanaotakiwa kuandikishwa shule na wawasisitize wazazi na walezi kufanya hivyo.

Alisema kila kundi litimize wajibu wake ili watoto wote waandikishwe, na kuendelea na masomo, katika ngazi husika.



Mkuu wa kitengo cha uchaguzi cha Chama Cha Mapinduzi (CCM), Cuthbet Midala (kulia), akimkabidhi Hatibu Mngeja fomu ya kuomba kuteuliwa na chama hicho, kugombea nafasi ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwenye ofisi za makao makuu ya CCM, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# RC Mtaka apongeza jiji kwa ubunifu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amelipongeza Jiji la Dodoma kwa kubuni mradi mkubwa wa soko la machinga, maarufu kama 'Machinga Open Market' kwa kutumia mapato yake ya ndani huku akiitaka kampuni iliyopewa zabuni ya kutekeleza mradi huo kukamilisha kwa wakati.

Pongezi hizo alizitoa jana jijini hapa wakati wa ziara ya kukagua eneo hilo na kulipongeza jiji kwa kubuni na kuanza ujenzi wa soko hilo katika eneo la Bahi Road jijini hapa. Katika ziara hiyo, Mtaka aliongozana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatuma Mganga, Mkurugenzi wa Jiji Joseph Mafuru, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na wataalamu kutoka Jiji na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

"Nikushukuru na kukupongeza Mkurugenzi wa Jiji kwa kuchukua hilo wazo. Wengi wanataka kuona makao makuu yanafananaje. Tunaenda kuwa na soko ambalo nchi hii nzima halmashauri 184 watakuja kujifunza ama kwa kupenda hata kama ni kimoyomoyo kwamba Jiji la Dodoma limekamilisha mradi huu mkubwa," alisema.

Katika hatua nyingine, Mtaka aliitaka Kampuni ya Mohammed Builders kuhakikisha inakamilisha ujenzi wa mradi huo ifikapo Machi 17, mwaka huu, ili kumpa zawadi Rais Samia Suluhu Hassan ya kutimiza mwaka mmoja tangu awe madarakani.

"Mnajua sababu ya kutaka Machi 17 muwe mmemaliza huu mradi ni kwamba siku hiyo Rais atakuwa anatimiza mwaka mmoja akiwa madarakani, hivyo nataka tumzawadie zawadi ya hili soko. Naamini litakuwa la kisasa na machinga hawatakuwa wakipata shida," alisema.

Mtaka pia alisema atawashirikisha wataalamu wote kuhakikisha soko hilo linajengwa kisasa na linakuwa na mahitaji yote ambayo binadamu anatakiwa kupata.

"Ndio maana wataalamu wote wapo hapa. Lengo langu tujenge kitu cha kueleweka hata baada ya miaka kadhaa lakini kubwa nataka halmashauri zote 184 zije zijifunze hapa namna ya kujenga soko bora la wamachinga. Hapa kutakuwa na kila kitu na litakuwa soko la saa 24," alisema.

Alilitaka Jiji la Dodoma baada ya soko hilo kukamilika kuwaondoa machinga wote waliopo katikati ya mji ili kuliweka jiji katika hali ya usafi. Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Mganga alilipongeza Jiji la Dodoma kwa kutenga asilimia 40 ya mapato ya ndani kujenga eneo hilo la wajasiriamali kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni saba huku akizitaka halmashauri zingine za mkoa huo kuiga mfano kwa jiji hilo.

Kiongozi kutoka Kampuni ya Mohammed Builders, Mohammed Halfaj, alimhakikishia Mkuu wa Mkoa kwamba mradi huo utakamilika muda ambao umepangwa.





# Rais Mwinyi asamehe wafungwa 29 Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ametoa msamaha kwa wafungwa 29 waliokuwa wakitumikia vifungo katika magereza ya Unguja na Pemba.

Msamaha huo umetolewa ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Taarifa iliyotolewa jana na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said, ilisema msamaha huo unatokana na uwezo aliopewa Rais chini ya kifungu cha 59 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Kutokana na msamaha huo, Rais Mwinyi aliamuru kuwa kifungo kilichobaki cha wafungwa walionufaika na msamaha huo, ambao bado wanaendelea kutumikia katika magereza waachiwe huru kuanzia Januari 11, 2022. Tayari wafungwa hao wameshaachiwa huru.

Msamaha huo ambao hutolewa kila mwaka katika kipindi cha sherehe za Mapinduzi, huwahusisha wafungwa ambao ni wazee sana, wenye maradhi sugu au wenye makosa madogo.

Wengine ni wale ambao wamebakisha muda mfupi wa kutumikia vifungo sambamba na kuonyesha nidhamu nzuri gerezani na kujutia makosa yao.

Wafungwa hao, maarufu kama wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo, wenye makosa kama vile kuua kwa makusudi, wizi wa kutumia nguvu, wizi wa mali ya umma, makosa ya kudhalilisha wanawake na watoto, dawa za kulevya na wenye makosa mengi ya zamani kwa kawaida huwa hawapewi msamaha.



Kaimu Jaji Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan Abdallah (katikati), akizungumza baada ya utiaji saini wa makubaliano ya ushirikiano kati ya Mahakama Kuu Zanzibar na Taasisi ya watetezi wa haki za binadamu Tanzania (THRDC), mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waandishi wafunzwa utatuzi migogoro

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAANDISHI wa habari wametakiwa kuwa sehemu ya kutatua migogoro ili kuifanya jamii kuwa na umoja na mshikamano hatimaye kusaidia kuondoa tofauti zilizopo hasa za kisiasa na kuharakisha maendeleo ya nchi.

Hayo yalielezwa jana na Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Zanzibar, Abdallah Mfaume, wakati akifungua mafunzo ya uandishi wa habari za utatuzi wa migogoro na ujenzi wa amani kwa waandishi wa habari katika ukumbi wa kitengo cha uzazi shirikishi Kidongo Chekundu, Zanzibar. Mafunzo hayo yanasimamiwa na Search for Common Ground kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya.

Alisema Zanzibar inakabiliwa na migogoro mingi ikiwamo ya ardhi, kijamii, kiuchumi, kidini na kisiasa na kwamba ikiendelea kukaa bila kuripotiwa katika vyombo vya habari, itashindwa kupatiwa ufumbuzi.

Waandishi wa habari, alisema hujikita zaidi katika uandishi wa habari za kisiasa kipindi cha uchaguzi hali inayochangia uwapo wa migogoro hiyo.

Alisema ikiwa wanahabari watatumia nafasi yao katika kupunguza migogoro hiyo, watakuwa wamechangia kwa kiasi kikubwa katika kuleta maendeleo nchini.

Lengo la mafunzo hayo, alisema ni kuhakikisha wanapewa taaluma juu ya utatuzi wa migogoro na kuisaidia jamii katika utatuzi huo.

Alisema waandishi wa habari ni watu muhimu katika jamii na wanaweza kutoa taarifa zao katika nchi na kupatiwa ufumbuzi.

"Taaluma ya utatuzi wa migogoro ni kuhakikisha mnatoa taarifa za migogoro mbalimbali ikiwamo ya ardhi, kijamii, kiuchumi na hata migogoro ya kisiasa na kuhakikisha inapatiwa ufumbuzi," alisisitiza.

Aliwataka wanahabari kuacha kuwa chanzo cha kuchangia migogoro katika jamii kwa sababu taaluma yao haiwataki kujihusisha na mambo hayo na badala yake watumie taaluma yao kutatua migogoro kwa kutoa taarifa na kufanyiwa kazi.

Akiwasilisha mada ya dhana ya migogoro na vyanzo vya migogoro, Mwezeshaji Ali Haji Mwadini, alisema Zanzibar imetoka katika migogoro hasa ya kisiasa lakini kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) mwaka 2010 kumesaidia kwa kiasi kikubwa kuwaunganisha Wazanzibari na kuwa kitu kimoja.

SUK, alisema ina manufaa makubwa kwa wananchi wa Zanzibar kuhakikisha wanaendeleza umoja, mshikamano na maelewano ili nchi iendelee kupiga hatua kubwa za kimaendeleo.

Aliwataka wanahabari kuendelea kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa serikali hiyo ambayo imetokana na maridhiano ya kisiasa.

"Msisubiri kuripoti SUK katika serikali pekee. Ni jukumu lenu pia kwenda chini kwa wananchi kuwaelimisha na kupata maoni yao ili kuona serikali yetu ya umoja wa kitaifa inaendelea kuleta matunda kwa wananchi wa Zanzibar," alisisisitiza.

Nao washiriki wa mfunzo hayo, walisema mafunzo waliyopewa yana umuhimu mkubwa kwao katika kuelimisha na kuibua changamoto zinazoikabili jamii na kuelimisha umuhimu wa serikali ya umoja wa kitaifa ambayo ina manufaa makubwa katika taifa.

## Kamati ya maadili mawakili yaundwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAIMU Jaji Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan Abdallah, amesema mahakama imeunda kamati ya maadili na nidhamu kwa mawakili na mahakimu kwa sababu baadhi yao ni tatizo katika usikilizaji wa mashauri mahakamani.

Jaji Abdallah aliyasema hayo jana Mahakama Kuu, Vuga mjini Zanzibar, baada ya hafla fupi ya utiaji saini wa makubaliano ya kurasmisha ushirikiano kati ya mahakama kuu na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC).

Makubaliano hayo yana lengo la kuhakikisha haki inapatikana, kuondosha malalamiko katika jamii na kushirikiana kufanya utafiti kuhusu matatizo yanayokabili mahakama na kuyafanyia kazi.

Alisema anapokea malalamiko mengi ya mawakili kupokea ujira wa kazi lakini kazi hizo hawazifanyi, hawatoi ripoti vizuri kwa wateja wao na kuwa chanzo cha kuairisha mashauri ya kesi, hivyo husababisha haki isipatikane mahakamani.

Kaimu Jaji Mkuu alisema kama kuna malalamiko yoyote kutoka kwa mahakimu au mawakili hawakutenda haki, aliwataka wananchi kupeleka malalamiko yao mahakamani ili kufanyiwa kazi.

"Kamati ya maadili kwa mawakili na mahakimu ipo na imeundwa kisheria, hivyo wananchi wanaweza kuleta malalamiko yao mahakamani," alisema.

Alisema safari ya maboresho ya mahakama inaendelezwa ili wananchi kuziamini mahakama na huduma kupatikana kwa urahisi.

Mahakama Kuu, alisema imedhamiria kufanya maboresho kwa sababu imekumbwa na matatizo mengi na imedhamiria kuyaondosha ili kupunguza malalamiko kutoka kwa wananchi.

Pia alisema makubaliano hayo yatasaidia kujenga uwezo wa kutoa haki katika jamii, kushirikiana katika mambo mbalimbali ikiwamo kufanya utafiti ambao utaainisha matatizo ya mahakama na jinsi ya kuyatatua.

Alisema pia makubaliano hayo watafaidika kupata mafunzo katika masuala ya kutenda haki, usimakiliza wa mashauri mahakamani kwa sababu kuna tatizo hilo la usimamizi wa mashauri na watu wanalalamika mashauri na hukumu hazitoki kwa haraka.

Mratibu wa THRDC Ofisi ya Zanzibar, Abdallah Ali Abeid, alisema makubaliano hayo yamefikiwa baada ya kufanya kazi nzuri na mahakama na kuamua kujirasmisha katika kushirikiana ili haki ipatikane mahakamani.

"Tumemaua kushirikiana na mahakama ili mfumo wa utoaji wa haki kuimarika na usharikiano huu utazaa matunda ndani ya miaka mitatu," alisema.

Naye Mtaribu wa THRDC Tanzania, Onesmo Olengurumo, aliipongeza serikali ya Zanzibar katika kusukuma gurudumu la maendeleo na wananchi kupata fursa ya kufika mahakamani kwa wakati na kupata haki wanazostahili.



TREY KAANZA VIBAYA 2022 Uk.14



Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



## SIKUBALI AMAPIANO

# AY anapotoa somo kiutu uzima

MJADALA kuhusu muziki mpya unaofahamika kama Amapiano, unazidi kushika kasi hatua ambayo imewagawa pande mbili wasanii wa muziki wa kizazi kipya.

Muziki huo wenye asili ya Afrika Kusini, umepata umaarufu nchini na baadhi ya wanamuziki wakubwa na wale wanaochipukia wamejikuta wakiupiga na kuusifia.

Hata hivyo, kuna baadhi wa wasanii wamejitokeza kuupiga vita wakitoa hoja kwamba muziki huo unaweza kuua Bongo Fleva na kujikuta wakipoteza vipaji vyao.

Wasanii kama Maua Sama na Ali Kiba, wameweka wazi kwamba abadan hawatapiga na hawawezi kufikiria siku moja wataingia katika mkumbo huo.

Mwanamuziki mkongwe hapa nchini Ambwene Yesaya, maarufu kama AY, ameingia katika mjadala huo baada ya kuhoji kama muziki huo umeleta tija kwa wasanii walioimba.

Ameuliza kama muziki wa Amapiano una biashara kwa wasanii wa Tanzania wanapokwenda nchini Afrika Kusini.

Amesema tofauti na wenzao wa nchi hiyo, ambao wanakuja kwa wingi na kujikusanyia pesa na kisha kurudi kwao.

Aidha, amewataka wadau wa muziki kujifunze biashara ya muziki kwa kufanya kila kitu ambacho kinaweza kuwaingizia pesa, badala ya sifa na umaarufu pekee.

"Wakuu, wasanii na Ma Dj waliokuwa bize kufanya Amapiano hapa Tanzania, mpaka leo nani kashaenda Afrika Kusini kuokota hela zao? Tujifunze biashara" ameandika katika ukurasa wake wa Twitter.

"Maana naona wasanii na Dj's wa South Africa wanavyokuja kuokota hela Bongo,nini shida".

## BASI SAWA

### Usiniache' ya Zabron Singers hatari tupu



HATIMAYE kundi la muziki wa Injili, Zabron Singers, limeachia video ya wimbo wao mpya 'Usiniache'ambao unaendelea kufanya vizuri.

Japhet Zabron ambaye ni mwandishi na mtunzi wa nyimbo za kundi hilo , ameliambiua BT kuwa wamekuwa na desturi ya kuandaa kazi mapema ili kuwapa furaha mashabiki wao.

"Usiniache ni wimbo unaofanya vizuri kwa sasa na tunamshukuru Mungu umeendelea kushika namba za juu kwenye chati ya muziki katika mtandao wa YouTube," amesema.

Aliongeza kwa kusema: "Tunamshukuru Mungu kwa kutufikisha mwaka mpya 2022 na habari njema ni kwamba mwaka huu kuna ujio wa albamu kutoka kwa baadhi ya waimbaji ndani ya kundi.

### Ibraah ebu kuwa na huruma



MAMBO yanazidi kwenda kasi, kwani mwanamke aliyepata mtoto na msanii kutoka Konde Gang, Ibraah amezidi kutoa malalamiko yake kwamba nyota huyo hana msaada kwa mtoto wake.

Kim Mishepu ambaye amekuwa na uhusiano na Ibraah kabla hajakuwa staa na kumzalia mtoto mmoja wa kike aitwaye Yasreen, amesema anazidi kuelemewa na malezi kutokana na baba yake kushindwa kutoa pesa za matunzo.

"Nimeamua kuweka wazi kila mtu afahamu kwamba Ibraah hana msaada wowote kwangu, mimi mwenyewe naumwa lakini hajali chochote, wakati mwingine napata wakati mgumu kwani sina kitu," amesema Kim.



## Kumbe Billnass anapenda wali maharage

MWANAMUZIKI wa muziki wa Bongo Fleva, Faustina Mfinanga maarufu 'Nandy' amefunguka chakula anachokipendelea zaidi mpenzi wake Billnas kuwa ni wali maharage nazi.

Mwanamuziki huyo ambaye amelamba dili nono la kuwa balozi wa nazi ya Azania 'Azania Coconut Cream'amesema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa bidhaa hiyo mpya kutoka katika kampuni ya Azania Group.

"Billnass anapenda sana wali maharage nazi, lakini sitaki sana kutoa siri za ndani asije mtu akapika wali maharage nazi bure ha ha ha " alisema Nandy

Nandy alisifia kiungo hicho cha nazi kuwa ni bora kuliko zingine alizowahi kuzitumia katika mapishi kwa kuwa kina virutubisho vya kutosha.

## Maisha ya Utata; Kila mtu atakula ulichopanda

**Na Adam Fungamwango**

MAISHA ya Utata' ni filamu yenye mafunzo mengi kwenye jamii kwa nyanja mbalimbali. Mtunzi hakulenga jambo moja, bali alitaka kuifundisha jamii vitu kadhaa ambavyo inabidi iwe navyo makini.

Kwa mabinti wanafunzi, filamu hii inawafundisha wafuatilie kwa makini masomo yao na si kujiingiza kwenye masuala mengine, ikiwemo mapenzi.

Kwa upande wa wazazi ina wafundisha wasiwe na miyo migumu. Ni kweli mara nyingi wanakutana na changamoto kubwa ambazo zinafanywa na watoto wao, lakini inabidi wawe wepesi wa kufanya maamuzi, na hata kusamehe.

Pia inafundisha jamii kuwa na roho nzuri. Roho njema ya kusaidia kama ukimkuta njiani mtu ni mhitaji, au kuna kitu umefanya njiani kwa bahati mbaya, saidia, omba msamaha, unaweza kuwa umefanya jambo ambalo wewe mwenyewe hujui kuwa linaweza kukusaidia.

Zamda ambaye ni mwanafunzi, lakini anaingia kwenye mahusiano na kijana Zumbe.Yalikuwa ni ya siri, lakini mimba ikawaumbua.


Zamda anatengwa na wazazi wake. Anatimuliwa na kwenda kuishi kwa Zumbe, ambaye kwa bahati nzuri hakuikataa mimba wala mpenzi wake.

Mzee Pandu ambaye ni baba wa Zamda, hakujishughulisha na chochote kile juu ya binti yake. Wakawa ni kama watu waliotengwa. Lakini kupendana kwao kukawa faraja. Hata hivyo hawakuwa na kitu chochote zaidi ya kubangaiza tu.

Rafiki ya Zumbe anatoka mjini kumfuata ili akafanye kazi. Hata hivyo inashindikana kwa sababu siku chache zilizopita akiwa na baiskeli, alimgonga bibi mmoja, akapoteza vyeti vyake wakati anakimbia.

Hata Zumbe alipokwenda kwa shangazi yake naye kutaka akae na binti aliyempachika mimba, alikataa katakata.

Zamda akakimbilia kwa bibi yake ili amuombee msamaha kwa baba yake. Hilo linafanyika, lakini wakati Zumbe anakuja kwenye kikao, bibi akamkumbuka kuwa ndiye kijana aliyemgonga na



# Kama kuachwa haliwahusu!

MAMA mtoto wa mwanamuziki wa Bongo Fleva, Rayvanny, amekasirishwa na tuhuma kwamba ameachwa akisema suala hilo haliwahusu wengine.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram,Fahyma maarufu kama Fahyvanny, amewataka watu kuacha kujadili uhusiano wake na Rayvanny na kwamba kama kuachwa au kutoachwa ni suala lake binafsi.

"Nasema hivi mnikome jamani Fahyma kaachwa kaachwa, nimechoka na kama sijaachwa je? na wewe unayeendelea kunichokonoa endelea kuna jambo unalitaka". ameandika



# Fasta wameachia ngoma 2022

**Na Adam Fungamwango**

MWAKA mpya wa 2022 umeanza na 'fasta' tu na baadhi ya wasanii wameshaanza kwenda nao sambamba kwa kutoa ngoma.

Wapo walioumaliza mwaka 2021 kwa kutambulisha ngoma zao ambazo zinatamba kama Platform TZ akimshirikisha Ruby na ngoma yao ya 'Vitamu' iliyotoka Desemba 17, Zuchu akimshirikisha Bountle Smith akitoa kitu kinaitwa 'Kitu', kikitoka Desemba 22 na mwishoni kabisa mwa mwaka jana Desemba 31, Mr Blue aliufunga kwa kutoa ngoma akimshirikisha Aslay, ngoma inaitwa 'Mpenzi Adui'.

Lakini kuna wasanii, tena wakubwa tu, mwaka ulipoanza wala hawakusubiri wala 'kulaza damu', wakaibuka na ngoma zao za kufungulia 2022. Wasanii hao ni hawa na ngoma zao ni hizi.

**Harmonize-Serious Love**

Katika hali inayoonyesha kuwa wasanii wa Kitanzania wameanza kubadilika taratibu, msanii Harmonize licha ya kutoa ngoma yake mapema tu 2022, Januari 2, lakini ameimba kwa lugha ya kingereza.

Inaonyesha kuwa wasanii wa Kitanzania wameanza kutaka kulishika soko la muziki nje ya nchi na hii ni baada ya kukubalika kwenye nchi kadhaa duniani.

'Serious Love', ndiyo wimbo uliofungua mwaka wa Harmonize.

**The Ben ft Diamond Platnumz-Why**

Simba, Diamond Platnumz, huwezi kumkosa kwenye shughuli kama hizi. Naye ni lazima aweke rekodi yake.

Safari hii amekuja kivingine. Ameshirikishwa na msanii The Ben kutoka nchini Rwanda kwenye singo ya 'Why', ambayo ipo kwenye lebo ya WCB. Ngoma hii imetoka Januari 4, siku nne tu baada ya kuingia kwa 2022.

Ni wimbo wa mapenzi ambao umeimbwa kwa lugha tatu, ya kiingereza, kiswahili na kinyarwanda.

**Killy ft Harmonize**

Msanii Killy, naye hakujiweka nyuma, ametoa ngoma yake mpya aliyoiita 'Ni wewe'. Ni wimbo wa mapenzi ambao ameutoa Januari 12, akimshirikisha 'Tembo', Harmonize ambaye anaonekana kama vile mwaka 2022 ameamua kufanya mambo makubwa ya kutoka na ngoma kibao pamoja na 'kolabo' za kutosha.

**Rayvanny-Rara**

Msanii Rayvanny ambaye mwenyewe anajiita Chui, naye ameingia kwenye orodha ya wasanii walioanza mwaka 2022 kwa kishindo baada ya kutoa singo yake iitwayo 'Rara'. Ameitoa Januari 5. Kama nilivyosema kuwa wasanii wa Kitanzania wanaangalia soko la ndani na nje, kwani wimbo huu pia ameimba kwa lugha ya kiswahili na kiingereza.

**Willy Paul ft Jux-Nimelewa**

Usidhani ni wimbo wa kilevi, hapana, ni wa mapenzi. Kuna mtu amelewa kwa mapenzi ya mtu. Ni Willy Paul ambaye amemshirikisha Jux kwenye ngoma 'Nimelewa'. Hii imetoka Januari 5 na kuwa mmoja wa wasanii wa mwanzo kuuanza mwaka 2022 vizuri kwa kutoa pini la ukweli.

basikeli na kushindwa kumpa msaada, akamkimbia. Bibi akabadilika na kusema kama ndiyo huyu hata yeye anapenga kupata msamaha.

Baada ya kuona mambo yanazidi Zumbe, akaamua liwalo na liwe, akamwambia laivu Zamda kuwa sasa ameamua kwenda mjini kutafuta maisha, maana kila analofanya linashindikana.

Zamda akiangalia atakaa na nani na mimba ile, hajui la kufanya kwani wazazi wamemtimua. Baada ya aliyempa mimba kuondoka, binti huyo akajitia kitanzi, akajiua.



# Momoa, Lisa wavunja ndoa yao



MWIGIZAJI nyota wa Marekani, Jason Momoa amempa talaka mke wake Lisa Bonet, baada ya miaka 17 ya ndoa yao.

Momoa aliandika katika ukurasa wake wa Instagram kwamba wameamua kuvunja ndoa yao huku wakiendelea kushirikiana katika mambo ya kifamilia.

Momoa na Bonet walianza uhusiano wa kimapenzi mwaka 2005, walifunga ndoa 2017 na katika maisha yao walipata watoto wawili.




## O Yeong-su won wa Squid Game kuwania tuzo

MSANII wa filamu ambaye amefanya vizuri katika tamthilia ya Squid Game, O Yeong-su won, ametajwa kuwa miongoni mwa watu watakaowania tuzo ya juu ya Golden Globe.

Su Won ambaye sasa ana miaka 77, amekuwa msanii wa kwanza kutoka Korean kutajwa katika tuzo hizo ambazo zinawaniwa na waigizaji maarufu duniani.

Katika filamu ya Squid Game, O Yeong-su amekuwa mshiriki mwenye umri mkubwa na ndiye aliyeonekana kuandaa mchezo huo ambao kimsingi huchezwa na watoto, lakini ulitengenezewa filamu iliyofanikiwa kupendwa duniani kote.

## Julia nguo tu ukarogeka

UMESIKIA alichofanya rapa Kanye West wakati akibembeleza mapenzi kwa Julia Fox? Basi unaambiwa msanii huyo bilionea ilimbidi kwenda dukani na kumnunulia shehena ya nguo mrembo huyo kabla ya kwenda kulala naye hotelini.

Kulingana na Fox wakati akifanya mahojiano na jarida moja, mwanamuziki huyo alifanya hivyo kama kumpa heshima kwa kumkubalia kuwa katika uhusiano..

"Inafurahisha kuona ndoto ya kila mwanamke inapokuwa kweli, ilikuwa kama kweli muda wa Cinderella.Sifahamu nini kilifanyika au yote aliyofanya katika muda ule," amesema.





## Trey kaanza vibaya 2022

MWANAMUZIKI wa Marekani, Trey Songz, ameanza vibaya mwaka 2022 baada ya kutuhumiwa kumbaka mchezaji wa mpira wa kikapu, Dylan Gonzalez.

Mrembo huyo ambaye alikuwa akichezea timu ya Nevada, alitoa tuhuma hizo kupitia ukurasa wake wa Instagram, akisema mwimbaji huyo nyota alimbaka na kumuambukiza ugonjwa wa zinaa.

"Alitumia nguvu na kunilazimisha kufanya naye mapenzi na kunisababishia ugonjwa, alinishika kwa nguvu kwa mikono yake wakati tukiwa hoteli ya Las Vegas," amesema.

## Doris hongera kuliimarisha penzi

MSANII wa filamu kutoka Nollywood, Doris Ogala, ameibuka na kuweka sawa uhusiano wake baada ya kusema bado yuko katika mikono salama ya mume wake.

Mwigizaji huo ameamua kuweka wazi suala hilo baada ya kuwepo na uvumi kuwa amepewa talaka na mume wake hivi karibuni.

Katika ujumbe aliouweka katika ukurasa wake wa Instagram, Doris amesema ndoa yake ipo imara na anaendelea kuishi katika nyumba moja na mume wake.



MAKALA

# SHUJAA PANYA MAGAWA

## ●Kazi yake imeokoa maelfu ya watu
## ●Dunia yaomboleza kifo chake

Na Mwandishi Wetu

NI nadra kusikia kifo cha mnyama kinaombolezwa dunia nzima. Pengine panya kutoka Tanzania anayeitwa Magawa, ameweka historia kwa kuwa maarufu na kifo chake kuombolezwa duniani kote.

Panya huyo mkubwa anayetambulika kama shujaa, alitumika kutafuta na kutegua mabomu ya ardhini na vilipuzi vingine katika nchi zilizokumbwa na vita.

Kifo cha Magawa kiliwashtua watu wengi na katika muda mfupi baada ya kutolewa tangazo lake, mitandao ya kijamii ilivamiwa na watu kwa ajili ya kuomboleza na kusifia kazi yake iliyotukuka.

Taarifa ya kifo chake ilitolewa katika ukurasa wa instagran unaomilikiwa na shirika la Apopo ambalo linaendesha mradi wa utafiti wa panya katika Chuo Kikuu cha Sokoine mkoani Morogoro.

"Magawa alikuwa na afya njema wiki jana, lakini afya yake ilianza kudhoofika mwishoni mwa wiki hii na kuaga dunia akiwa na umri wa miaka minane," ilisema taarifa hiyo.

Katika uhai wake, panya huyo alisaidia kugunduliwa kwa zaidi ya mabomu 100 ya kutegwa ardhini nchini Cambodia.

Kutokana na mchango wake huo na kunusuru maisha ya maelfu ya watu, Septemba 2020, alikabidhiwa Medali ya Dhahabu ya PDSA, ambayo ni tuzo ya juu zaidi ya ushujaa ambayo mnyama anaweza kupokea.

Hata hivyo, mwaka jana Magawa alistaafu na panya mwingine anayeitwa Ronin alichukua nafasi yake.

Pamoja na kuzaliwa na kukulia Tanzania, panya Magawa alikufa akiwa nchini Cambodia na mazishi yake yalifanywa hukohuko.

**SIRI YA PANYA MAGAWA**

Kulingana na watafiti kutoka Apopo, panya huyo mkubwa kutoka Afrika, alikuwa na uwezo mkubwa wa kubaini mabomu ya kutegwa ardhini.

Magawa ameweza kunusa mabomu 70 na silaha 38 ambazo hazijalipuka katika maisha yake.

Shirika la matibabu ya wanyama la Uingereza lisilokuwa la kiserikali (PDSA) lilimtuza medali ya dhahabu kutokana na kujitolea kwake kuokoa maisha kupitia kazi yake ya kubaini mabomu hatari yaliyotegwa ardhini nchini Cambodia.

Ndani ya nchi hiyo, inadhaniwa kuna mabomu zaidi ya milioni sita yaliyotegwa ardhini.

Panya huyo ambaye ana umri wa miaka nane mpaka anapoteza uhai wake, alipewa mafunzo na shirika lisilo la kiserikali la Apopo kutoka Ubelgiji, makao makuu yake yapo Tanzania. Shirika hilo limekuwa likiwalea wanyama wanaofahamika kama Panya buku ambao wana uwezo wa kugundua uwepo wa mabomu ya kutegwa ardhini.





> **Magawa ameweza kunusa mabomu 70 na silaha 38 ambazo hazijalipuka katika maisha yake.**

Wanyama hao wanafuzu baada ya kuwapa mafundisho.

Ofisa Mkuu Mtendaji wa Apopo, Christophe Cox, amesema kifo cha Panya Magawa kimewapa nguvu ya kuwafundisha wengine, mpaka sasa wana panya 20 ambao wameanza kufundishwa na wanaonyesha matokeo mazuri.

Kulingana na Apopo, Magawa alizaliwa na kulelewa Tanzania akiwa na uzani wa kilo 1.2 na urefu wa senti mita 70.

Japo ni mkubwa kuliko spishi zingine za panya, Magawa ni mdogo na mwepesi kiasi kwamba hawezi kulipua mabomu akitembea juu.

Panya hao wanafundishwa kubaini kemikali iliyotumiwa katika vilipuzi, wanaweza kunusa na kugundua mabomu kwa haraka zaidi.

Magawa peke yake alikuwa na uwezo wa kusaka mabomu katika eneo lenye ukubwa wa uwanja wa mpira wa tenesi kwa muda wa dakika 20 pekee, jambo ambalo Cox anasema lingemchukua mtu mwenye kifaa cha kubaini vifaa vya chuma kati ya siku moja hadi nne.

Ili aweze kufuzu mafunzo, panya inawachukua takriban mwaka mmoja kabla ya kuwa na uwezo wa kugundua mabomu yaliyotegwa ardhini.

Panya huyo alikuwa na uwezo kutumia saa moja na nusu kwa siku nyakati za asubuhi kufanya kazi.

Mkurugenzi Mkuu wa PDSA, Jan McLoughlin anasema kazi yake katika shirika la Apopo ilikuwa ya kipekee na ya kuridhisha.

"Kazi ya Magawa imeokoa na kubadilisha maisha ya binadamu ambao wanaathiriwa na mabomu hayo ya kutegwa ardhini. Kila uvumbuzi alioufanya umepunguza hatari ya kujeruhiwa au kufariki kwa watu." anasema

Kwa mujibu wa shirika lisilokuwa la kiserikali la kuondoa mabomu nchini Cambodia ( HALO Trust), zaidi ya watu 64,000 walijeruhiwa na wengine 25,000 kukatwa viungo vya mwili kutokana na milipuko ya mabomu ya kutegwa kuanzia mwaka 1979.

# Watanzania asilimia 60 kupatiwa chanjo corona

## •Elimu yaondoa hofu, mashaka kwa jamii




Ofisa Afya Manispaa ya Itigi, mkoani Singida akitoa chanjo katika Kampeni ya Mpango Shirikishi na Harakishi Awamu ya Pili, iliyotekelezwa katika mikoa mbalimbali nchini mwishoni mwa mwezi Desemba mwaka jana. Kampeni ililenga kuwafikia wananchi katika maeneo yao ya kazi, biashara na nyumbani. **PICHA: Mary Geofrey)**

**Na Mary Geofrey**

TAKWIMU zinaonyesha kuwa, hadi kufikia Desemba 18, mwaka jana, jumla ya watu 1,275,795 wamepata chanjo ya UVIKO-19 sawa na asilimia 2.21 ya Watanzania wote.

Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichwale, anaeleza takwimu hizo zilitolewa Desemba 21, mwaka jana, wakati wa semina ya Uhamasishaji na Utoaji wa Chanjo kwa Wataalamu wanaotekeleza Mpango Harakishi na Shirikishi Awamu ya Pili, unaotekelezwa na Wizara ya Afya, Kitengo cha Elimu kwa Umma.

Dk. Sichwale anasema hadi mwezi Desemba mwaka jana, kupitia ushirikiano na mashirika mbalimbali (COVAX Facility) na wadau wa maendeleo ambapo nchi ilipata chanjo kwa asilimia 20 ya wananchi na mpaka sasa jumla ya dozi 4,421,540 zimeingia nchini.

"Juhudi mbalimbali zinaendelea ili kuweza kupata kiasi cha chanjo kitakachowezesha kuchanja asilimia 60 ya wananchi ambacho kitawezesha kufikia kiwango cha kinga kinachohitajika kulinda jamii yote,"anasema.

> **4,000**
>
> **Anasema kila mkoa utatakiwa kuchanja watu 4,000 hadi 5,000 kwa siku ili kufikia lengo la kuchanja asilimia 60 ya Watanzania.**

Naye Katibu Mkuu, Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi, anasema mpango huo, Harakishi na Shirikishi Awamu ya Pili wa Kampeni ya Uhamasishaji na Utoaji Chanjo ya UVIKO-19, unalenga kuchanja watu 80,000 hadi 100,000 kwa siku.

Anasema kila mkoa utatakiwa kuchanja watu 4,000 hadi 5,000 kwa siku ili kufikia lengo la kuchanja asilimia 60 ya Watanzania.

Anasema awamu ya kwanza ya mpango huo, walikuwa wakichanja watu 20,000 hadi 40,000 na ndio sababu ya kuanzisha mpango huo harakishi na shirikishi.

"Mpango huu utahusisha mitaa na nyumba kwa nyumba na pamoja na kuhamasisha chanjo, wataalamu wa afya, watatoa huduma za kupima na matibabu kwa wagonjwa waliopatikana na magonjwa," anasema.

Aidha, anasema tafiti zinaonyesha kuwa, asilimia 70 ya Watanzania wapo tayari kuchanja chanjo ya UVIKO-19.

Anasema pia kwa upande wa Afrika, utafiti unaonyesha asilimia 70 hadi 80 wapo tayari kupata chanjo ya UVIKO-19.

Anasema wameanza kufanya Utafiti wa Chanjo wa UVIKO-19 na magonjwa mengine nchini.

Prof. Makubi anasema Wizara ya Afya, pia inaendelea kutoa elimu kwa jamii ili ielimike na kuanza kuelimishana wenyewe katika kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huo.

Anaeleza serikali imetumia mfumo wa afya na serikali za mitaa kuhakikisha elimu inawafikia moja kwa moja wananchi na kupata chanjo.

"Kupitia elimu inayotolewa watu wanaelimika bila kufunga mipaka ya nchini na shughuli za uchumi zinaendelea," anasema Prof. Makubi.

Anasema awamu ya kwanza ya mpango huo, ilifanikisha watu kujitokeza kwa wingi kupata chanjo na kusababisha chanjo za Johnson & Johnson kumalizika kwa wakati.

> **60%**
>
> **Aidha, Prof. Makubi, anasisitiza serikali ina nia njema ya kuwatakia afya njema Watanzania kwa kuhakikisha wanachanja kwa asilimia 60.**

Anasema kwa sasa kuna aina mbili za chanjo na kuwaonyesha wananchi waendelee kuchanja ambazo ni Pfizer na Morderna.

"Hatua hii inaonyesha kuwa Rais Samia anawapenda Watanzania na kuwaona wananchi wanakuwa na afya njema, tumefanya kuwa harakishi kwa sababu ugonjwa wenyewe ni haraka na unaua watu kwa haraka," anasema Prof. Makubi.

Anawahimiza pia kuwapa moyo wananchi na kuwaonyesha umuhimu wao katika kupata chanjo na faida zake.

**HAKUNA LENGO BAYA**

Aidha, Prof. Makubi, anasisitiza serikali ina nia njema ya kuwatakia afya njema Watanzania kwa kuhakikisha wanachanja kwa asilimia 60.

"Hakuna chanjo iliyofanikiwa kwa kulazimisha bali kwa kuelimishana na wananchi na kuelewa sayansi, hivyo baadae mtu kuamua kuchanja Kwa hiari yake," anasema Prof. Makubi.

Anasema kampeni hiyo itaenda kuwatumia viongozi wa mitaa wenyewe na kwamba kampeni ya mtaa kwa mtaa, haileti ulazima bali ni kupeana elimu ngazi ya mtaa na wananchi kwa hiari yao kwenda kuchanja .

Prof. Makubi anaongeza kwamba licha ya chanjo bado wananchi wanatakiwa kuendelea kuchukua tahadhari kwa kunawa mikono mara kwa mara kwa maji tiririka na sabuni, kuepuka misongamano na kuvaa barakoa.

"Jambo jingine niwakumbushe wananchi kufanya mazoezi pamoja na kula lishe bora, kwani mazoezi ni muhimu na inasaidia mifumo ya hewa kuwa mizuri," anasisitiza Prof. Makubi.

Naye, aliyekuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe, anasema ni muhimu kushirikishana na viongozi wa dini, mitaa na kimila ili kuwa na namna bora ya kuwafikia wananchi ili kuwalinda wazee waliopo majumbani.

Kadhalika aliwataka viongozi hao kuendelea kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa chanjo ya UVIKO-19 na kuendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa huo.

Hali ya ugonjwa nchini

Aliyekuwa Waziri wa Afya, Dk. Dorothy Gwajima, anasema maambukizi ya UVIKO-19 yanaongezeka nchini, hivyo wananchi wanatakiwa kuendelea kuchukua tahadhari.

Ametolea mfano idadi ya sampuli zinazopokelewa Maabara Kuu ya Taifa ni 47 kwa siku, tofauti na siku za nyuma zikiwa zinapokelewa sampuli 14 kwa siku, hali inayoonyesha idadi ya maambukizi inaongezeka.

Dk. Gwajima anasema, wananchi wamekuwa hawachukulii suala hilo kwa uzito unaotakiwa na ndio sababu hawaendelei kuchukua tahadhari.

"Kasi ya kujikinga na maambukizi bado ni ndogo licha ya kuwa wananchi wanaendelea kuchanja bado wanahitaji msukumo," anasema Dk. Gwajima.

Akizungumzia hali ya wagonjwa wa UVIKO-19, anasema kati ya wagonjwa 10 wanaofariki dunia, saba kati yao ni wale ambao hawajachanja na wengine watatu ni wale waliochanja lakini walizidiwa na magonjwa mengine kama shinikizo la damu, kisukari na wazee.

"Tunataka tusikilizane kila mtu achukue tahadhari na serikali haitaki kutumia nguvu kuwasihi wananchi na kutoa makatazo ya kusherekea Sikukuu, bali jamii inatakiwa kuchukua tahadhari zote," anasema.

## Mji wa kale uliozama baharini watafutwa

**MOMBAI,** INDIA

MJI wa kale wa India ulioitwa Dwarka, unaosemekana kuzama chini ya Bahari ya Arabia, umeanza kutafutwa na wana akiolojia wa chini ya maji.

Kazi inayotazamiwa ni utafutaji wa misingi ya kuta zake za jiji hilo ili kuthibitisha uwepo wake.

Mji huo ulikuwa moja ya vituo saba vya hija takatifu nchini humo, pia Dwarka sio tu kwa umuhimu wa kidini, bali pia kwa akiolojia.

Taarifa za zamani za mji huo, unaojulikana katika Epic Mahabharata kama ufalme wa kale wa Krishna, ilienea karibu kilomita 84 kama jiji lenye ngome ambapo Mto Gomti na Bahari ya Arabia hukutana.

Kulingana na maandishi hayo, mji huo wa zamani ulizama chini ya Bahari ya Arabia baada ya kifo cha Krishna.

Katika nusu ya pili ya karne iliyopita, wanaakiolojia walifanya majaribio ya kupata uthibitisho wa kimwili wa mji huo uliozama karibu na pwani ya Dwarka ya sasa ili waweze kuthibitisha kuwepo kwake bila shaka.

Matokeo yake, vitu vingi vya kale vimegunduliwa chini ya maji kama vile mawe na nguzo, hata hivyo, umri kamili wa matokeo yake bado unajadiliwa.

Wana akiolojia wanapanga kuchimba chini ya maji ili kutafuta misingi ya kuta za mji huo wa kale. Iwapo watapata eneo kamili la makazi hayo, utakuwa na umuhimu mkubwa wa kihistoria ya India.

**BBC**

## Al Shaabab yaitishia Kenya

**NAIROBI,** KENYA

KUNDI la Al-Shabaab limetishia kufanya mashabulizi zaidi nchini Kenya ili kulipiza kisasi kutokana na uwepo wa wanajeshi wake ndani ya Somalia.

Kitengo cha habari cha Al-Shabaab, kilisema hilo katika video fupi mpya iliyotolewa jana na kusambaa katika mitandao ya kijamii ya Rocket Chat na Telegram.

"Tunatuma salamu kwa Kenya, tumefunga safari ambayo haina kurudi nyuma, hizi ni nyakati za mwisho." Ilisema taarifa hiyo.

Chombo cha habari kinachohusishwa na kundi hilo kimedai hivi majuzi kwamba wanamgambo hao walizidisha mashambulizi yao nchini Kenya katika wiki za hivi karibuni kuelekea mwaka mpya.

Tangu Januari 3 mwaka huu, takriban watu 13 wameuawa katika mashambulizi yanayoshukiwa kufanywa na Al-Shabaab katika mikoa ya pwani ya Kenya iliyo jirani na Somalia.

Al-Shabaab imekuwa ikifanya mashambulizi nchini Kenya tangu mwaka 2011, wakati wanajeshi wa nchi hiyo walipovuka mpaka na kuingia Somalia kupambana na kundi hilo la kigaidi.

**DW**

# Raia waliokimbia chanjo warudishwa Rwanda

**KIVU,** DRC

RAIA 100 wa Rwanda ambao walikimbilia kisiwa kilichopo ziwa Kivu katika nchi jirani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, kuepuka kupata chanjo ya Corona wamerudishwa nchini kwao.

Hata hivyo, watu wawili wanadaiwa kutoonekana katika kundi hilo huku operesheni ya kuwasaka ikiendelea.

Ofisa wa Kisiwa hicho cha Idjwi, Roger Ntambuka, aliiambia BBC kwamba mamlaka iliweza kufanya mazungumzo na Wanyarwanda hao ili kuwarejesha nyumbani kwao.

"Hakukuwa na sababu ya Wanyarwanda hawa kubaki hapa. Tuliweza kuwashawishi," alisema.

Alisema raia hao ni wanawake, wanaume na watoto, walio ondoka kuelekea nyumbani kwa boti.

Gavana wa jimbo la magharibi mwa Rwanda, alisema hakuwa na habari kuhusu watu hao waliokimbia na haijabainika kama mamlaka ilihusika katika kuwarejesha nchini kwao.

Wiki iliyopita mamlaka ya Burundi iliwafukuza zaidi ya Wanyarwanda 10, waliokuwa wameingia nchini humo kukwepa chanjo ya lazima ya corona na kuwarudisha nyumbani.

Raia wa Rwanda lazima wapewe chanjo ili kuruhusiwa kutumia usafiri wa umma, kwenda kwenye maeneo ya starehe na migahawa au kuhudhuria hafla za umma.

**BBC**




Waumini wa Kihindu wakiwa katika hali mbaya ya kubanana wakati walipowasili kwa ajili ya hija ya kidini katika mto Ganges katika kisiwa cha Sagar, jimbo la Bengal magharibi nchini India jana. **(PICHA: REUTERS)**

# Polisi yawakamata watu wanne wakidaiwa kula nyama za watu

**ABUJA,** NIGERIA

POLISI katika jimbo la Zamfara kaskazini-magharibi mwa Nigeria, wamewakamata watu wanne wanaodaiwa kuhusika na ulaji nyama za watu na kuuza sehemu za binadamu.

Kamishna wa Polisi katika jimbo hilo, Ayuba Elkanah aliwaambia waandishi wa habari kwamba washukiwa hao walikamatwa baada ya maofisa wa upelelezi kupata maiti katika jengo ambalo halijakamilika, huku baadhi ya sehemu za mwili zikiwa zimetolewa.

Ugunduzi huo ulitokana na harakati za kufanya uchunguzi wa kupotea kwa mvulana wa miaka tisa.

Washukiwa hao wakiwemo wanaume watu wazima wawili na wavulana wawili, walikamatwa wiki iliyopita na washukiwa wengine wa genge hilo bado wanasakwa.

Mkuu huyo wa polisi alisema hadi sasa uchunguzi umebaini kuwa mara mbili kiongozi wa genge hilo aliwalipa washukiwa wengine watatu kiasi cha Naira laki tano kwa ajili ya kupata sehemu za binadamu.

Kuhusika na uuzaji wa sehemu za binadamu na ulaji nyama si jambo la kawaida katika jimbo la Zamfara. Lakini ni moja wapo ya maeneo ya Nigeria yaliyokumbwa na wimbi la mauaji na utekaji nyara kwa ajili ya fidia na magenge yenye silaha.

Hata hivyo, serikali inakabiliwa na ukosoaji kwa kushindwa kukabiliana na ghasia hizo.

Hata hivyo, wakati wa mkutano huo Kamanda Elkanah, alisema vikosi vya usalama pia vimewaokoa watu kumi na saba waliotekwa nyara hapo awali kutoka jimbo jirani la Niger na kupelekwa Zamfara.

Alisema vikosi vya usalama vilivyokuwa kwenye doria pia vimefanikiwa kupata baadhi ya silaha ikiwa ni pamoja na vifaa vya kurusha roketi kutoka kwa genge moja baada ya makabiliano ya risasi karibu na msitu.


Wiki iliyopita, takriban watu 200 waliripotiwa kuuawa wakati wa msururu wa uvamizi katika vijiji kadhaa jimboni humo.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**MUSSA JUMA MUSSA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1172-0028 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya NIANJEMA mwaka 2017,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **PWA/BAG/RB/18795/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**RAHMA OTHMAN MLINGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0622-0062 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia KUNDUCHI GIRLS ISLAMIC HIGH SCHOOL mwaka 2014,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi **Polisi taarifa DAR/URA/RB/20614/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

EDNA LUCAS TARIMO anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA HILUX yenye namba za usajili T 483 CFC chasis nambaYN850005943,engine namba 2Y0516998,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa KIL/MOS/RB/18067/2022

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

BERIT MARIE SKAARE anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA X TRAIL yenye namba za usajili T 507 CSE,chasis namba TNT31001204,engine namba QR25471813A,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa IRI/IRI/RB/17000/2022

## TAARIFA YA KUFUNGA KAMPUNI MWASHA JOJE LTD

Tunapenda kuutarifu umma kuwa katika kikao cha bodi cha wakurugenzi kilichofanyika tarehe 20/12/2021 kiliazimia kufunga kampuni ya MWASHA JOJE LTD yenye namba za usajili NO.123485 kuanzia tarehe 20/12/2021,kwa maelezo au madai wasiliana na 0784470615 au 0715470615

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HADITHI

# HADITHI

DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani. Aliwababaisha, kuwaliza, na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao alikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati. Alichojua wengi wanamfuata kama nyuki wafuatavyo ua zuri la waridi. Aliacha muda uongee. Alijua mwisho wa siku atajulikana ni nani anayependa uzuri na urembo wake na nani anampenda kwa dhati. Aliyempenda yeye kama yeye na si urembo wake. Fuatilia mtiririko huu wa riwaya hii kabambe, yenye kusisimua na mafunzo kwa jamii.

# Operesheni Namba Moja-9

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

"Karibu kijana."

"Ahsante Mjomba."

"Kama ulivyosikia, Diana ametekwa." Ilikuwa ni sauti ya upole ya mjomba wake Diana.

"Ndiyo mjomba, ndiyo maana nimekuja tujue nini tutafanya."

"Jana usiku wa manane, wakati sijui ni nani amemteka au kwa sababu gani. Kuna meseji imeingia kuwa hawa watekaji wanahitaji kiasi cha shilingi milioni hamsini ili wamuachie.

Jan alishtuka. "Milioni hamsini?"

"Ndiyo na wamesema nisilipeleke suala hili polisi na wao wana mtandao mpana sana, nikienda tu kuwaambia polisi watamuua mara moja. Kwa hiyo hapa sijui nifanye nini. Bora umekuja mjomba tushauriane."

Wakati akishauriana simu ikaita kwenye namba ambazo zilionekana kama siyo za nchi hii.

Mikono ya mjomba ikatetemeka, lakini haikumzuia kubonyeza kitufe ambacho kitafanya sauti isikike kwa wote.

"Hallo we mzee, binti yako tunaye hapa, tumekwambia utupatie shilingi milioni hamisini na tunakupa siku tatu kutoka leo. Binti yako ni mzima, hana tatizo lolote, lakini baada ya siku tatu kama hukutekeleza tutamchinja na maiti yake tutaitupa kule Mabwepande, tena tukiwa tumeikata vipande vipande kama mishikaki. Hebu kwanza ongea na mwanao hapa." Jan na Mjomba wake Diana waliisikia sauti hiyo nzito iliyoonekana haikuwa na mzaha. Pamoja na hayo, ilionekana kabisa mtu huyo aliongea akiwa kama ameweka kitu mdomoni kama pipi, au bazoka. Na hii inaonekana ni kuficha uhalisia wa sauti yenyewe ili isitambulike.

"Mjomba, mjomba, naumia mimi, nateseka, najua huna hizo pesa, lakini hebu fanya kila njia ili uniokoe, wamenitesa sana..." Ilikuwa ni sauti ya Diana. Kila mmoja alifahamu licha ya kwamba iliongea kwa shida, ikionekana kabisa ni kama ameteswa au kutopewa chakula kwa muda. Pili ni kwamba inaonekana alikuwa anataka kuendelea kuzungumza, lakini sauti ikakatwa. Nadhani kilichokuwa kinatakiwa kusikika ni sauti ya Diana ikisisitiza mjomba wake atoe hizo pesa, pia udhoofu wa sauti ili kumfanya Mjomba aharakishe kufanya alivyoamriwa, kwani ilionekana kabisa kuwa mpwaye yupo kwenye hali mbaya.




**"Kabla ya kukutana na wewe, tayari nina uhusiano na wanaume wengine wawili." Alikumbuka maneno aliyowahi kuambiwa na Diana.**

"Tufanyeje?" mjomba aliuliza katika hali ya kuchanganyikiwa.

"Itabidi tufanye kitu." Jan alijibu.

"Mimi pamoja na kwamba siko vibaya sana kimaisha, lakini shilingi milioni hamsini ni pesa nyingi sana. Yaani uwezo wangu wote hapa wa kutoa ni shilingi milioni 10 tu. Hapo ndiyo nimetoa na itachukua muda mrefu hadi hali yangu ya kimaisha irudi vizuri."

"Ni kweli mjomba, hebu na mimi niachie kwanza, niondoke hapa nikahangaike ili tuangalia nini tunafanya, maana siku tatu ni chache sana kwa pesa hizi wanazodai."

Ilibidi mjomba, ambaye jina lake halisi ni Ken amtazame kwa mshangao Jan. Alionekana ni kijana wa kawaida tu wa mitaani. Na anamfahamu kuwa aliletwa na Diana baada ya kumsaidia kwenye sakata la kuporwa mkoba wake. Hakudhani anaweza kuwa na msaada wowote kwenye jambo lile, hasa wa kipesa nyingi kama zile.

"Ina maana..."

"Mjomba wewe tulia, hili suala ni letu wote, siwezi kukuachia peke yako, hata kama sina pesa, ngoja niondoke, tutawasiliana baadaye."

************************************

"Kinachotakiwa hapa ni wewe kutoa shilingi milioni hamsini kama kweli unampenda Diana."

"Sawa ni kweli nampenda, lakini hizo ni nyingi sana ndugu yangu."

"Humpendi, haiwezekani mwanamke unayempenda, tena mrembo kama Diana, pesa hiyo iwe nyingi sana kwako na unaonekana una pesa nyingi kuliko hizo." alikuwa ni Jan akibishana na Chala.

Hao wawili walifahamiana baada ya kutambulishwa na Diana. Anakumbuka kuwa aliambiwa kuwa asiwe na wivu, kwa sababu hao wengine yuko nao kwa sababu maalumu na si kwamba ana mapenzi ya dhati kwao.

"Kabla ya kukutana na wewe, tayari nina uhusiano na wanaume wengine wawili." Alikumbuka maneno aliyowahi kuambiwa na Diana.

"Utanisamehe sana kwa sababu siyo kosa langu. Usikasirike, mimi nimekwambia hivyo nina maana yangu. Sikutaka kukuficha chochote kile. Nilikuwa na uwezo wa kusema sina mtu yoyote na ningeweza kukuficha kwa kipindi ambacho mimi nahitaji nikufiche." Maneno hayo yalikuwa yanajirudia kwenye ubongo wa Jan, huku akimtazama Chala.

"Ni hivi mpenzi. Siyo kosa langu ni Mungu amepanga hivi, sina uwezo wa kutengua. Ningeanza kukutana na wewe, hawa wawili nisingekuwa nao. Lakini nilikutana na mwanaume mmoja mfanyabiashara anaitwa Chala katika mazingira ambayo mimi sikuwa na mpenzi yoyote, achana na hawa wanaonifuatafuata. Halafu huyu mwingine ni askari anaitwa Marco, nilimpata nilipopata ajali ya bodaboda. Kwa bahati mbaya wewe nimekupata mwishoni. Na wewe ndiye nakupenda zaidi yao."

Ingawa ni maneno ambayo ambayo yalimtia simanzi sana Jan, lakini kwa mbali alianza kuona faida yake

"Jan, usiwe mnyonge, jione ni mshindi kwa sababu umewashinda wote. Sikuwa na sababu tena ya kuwa na mwanaume mwingine, lakini nimekukubali wewe. Umewapiku wao, usiwe na wasiwasi. Ila ninachokuomba ikitokea siku yoyote ile ukiona nipo na mmoja wapo. Basi wewe nitakutambulisha au ujitambulishe kuwa ni mjomba wangu. Yaani ni mdogo wa mjomba wangu kuanzia leo, hadi hapo malengo yangu yatakapokamilika."

Maneno hayo yote sasa aliyakumbuka na yalianza kuonekana yanaleta maana ya kile ambacho kilikuwa kinazungumzwa.

Jan aliona ni kweli kama Diana angemficha na bila kusema lolote lile, ikiwemo kumtambulisha kwa Chala kama mjomba wake, na siku hiyo Jan ilibidi awe mpole, asingeweza kumpata leo hii.

Wakati Chala alijua kuwa yupo na mjomba wa mpenzi wake aliyemfuata ofisini mwake, Jan alitambua kuwa anayezungumza ni mume mwenzake. Lakini hapo alikuwa anajifanya mjomba Diana alivyowahi kumtambulisha kwake.

"Hapana, hizo pesa zinaweza kufilisi kampuni yangu, kwa sababu inaingia shoti na itachukua muda kulilipa mjomba."

"Kwa hiyo wewe una shilingi ngapi ili tukamkomboe Diana."

"Nitatoa shilingi milioni kumi na tano tu."

"Poa lete tu hizo hizo, lakini mpenzi wako akijua kama umetoa kiasi hicho cha pesa, sijui kama mtaelewana tena."

"Unasikia mjomba, mimi nimetoa kiasi hicho, Diana naye ana ndugu zake ambao ndiyo nyinyi, wote inabidi tushirikiane kwa michango ili tufanikishe suala hili." Chala alijibu.

"Haya, zinatakiwa pesa keshi hapa, jamaa hawataki kuwekea kwenye akauti kwa kuhofu watajulikana na kukamatwa."

"Sawa mjomba."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# SIMBA QUEENS YASHUSHA WACHEZAJI WAPYA WAWILI

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kuongoza kwenye Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania na kuonekana haina mpinzani, Simba Queens imeongeza nguvu kwa kusajili wachezaji wapya wawili, Tagoe Amorkor kutoka Ghana na Amina Ramadhani, ikiwa ni saa chache kabla ya dirisha dogo la usajili kufungwa.

**Simba imetangaza rasmi kuwatambulisha wachezaji hao kwa ajili ya kuhakikisha msimu huu wanatetea tena ubingwa wa ligi hiyo wanaoushikilia.**

Hata hivyo, Amina ambaye ni kiungo mshambuliaji na nahodha wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), ni mchezaji anayerejea tena kwenye klabu hiyo baada ya kuwapo mwaka 2019, na alipachika bao kwenye mechi ya 'dabi' Simba Queens ikiigaragaza Yanga Princess mabao 7-0, mechi iliyochezwa Januari 2019.

Amina pia alikuwa kwenye kikosi cha Yanga Princess kilichochapwa mabao 4-1 katika mechi ya mzunguko wa kwanza msimu huu ambayo ilichezwa Januari 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Lakini kiungo huyo aliondoka na sasa anarejea tena, huku Mghana huyo ambaye ni straika taarifa zinasema ameletwa kwa ajili ya kumsaidia, Opah Clement katika safu hiyo ya ushambuliaji.

Katika Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania msimu huu inayoendelea, Simba Queens iko kileleni tangu kuanza kwa ligi hiyo inayoshirikisha timu 12, kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.

Simba Queens yenye pointi 15 imeshinda mechi zake zote tano ilizocheza na kupachika mabao 33 huku ikiruhusu nyavu zake kutikiswa mara mbili.

Nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo inashikiliwa na Fountain Gate Princess yenye pointi 10 sawa na JKT Queens huku nafasi ya nne ikikamatwa na Baobab Queens yenye pointi tisa, Alliance Girls yenye pointi nane inafuatia.

The Tigers Queens ya Arusha iko katika nafasi ya sita ikiwa na pointi saba sawa na Yanga Princess inayonolewa na Edna Lema.

Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania inatarajiwa kuendelea tena kesho kwa TSC Queens kuwakaribisha Simba Queens wakati Baobab Queens itacheza dhidi ya Oysterbay Girls huku keshokutwa Mlandizi Queens itaikaribisha Yanga Princess na Tigers itawafuata Ilala Queens.

# Azam FC kuhamishia hasira Bara

**Na Saada Akida,** ZANZIBAR

BAADA ya kupoteza mechi dhidi ya Simba katika michuano ya Kombe la Mapinduzi, Kocha Mkuu wa Azam FC, Abdihamid Moallin (pichani) amesema sasa nguvu zao wanazielekeza katika mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mbeya Kwanza.

Mbeya Kwanza itaikaribisha Azam FC kutoka Dar es Salaam katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Januari 18, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.



Akizungumza na gazeti hili jana, Moallin alisema fainali dhidi ya Simba ilikuwa na ushindani mkubwa na imempa mwanga mzuri wa kuona mapungufu ya kikosi chake na sasa atayafanyia kazi kabla ya kukutana na Mbeya Kwanza.

Moallin alisema anaamini michuano ya Mapinduzi imemsaidia pia kukiimarisha kikosi chake na sasa watarejea kwenye ligi wakiwa na 'moto'.

"Tumepokea matokeo na sasa tumerejea nyumbani kuhakikisha tunaendelea kufanyia kazi mapungufu yetu, lengo letu ni kuhakikisha tunapata matokeo mazuri katika mchezo huo unaokuja wa ligi," alisema Moallin.

Alisema kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake kilikuwa kizuri na ana matarajio makali hayo watayahamishia kwenye ligi ili kupata matokeo chanya.



Wachezaji wa timu ya kikapu ya Benki ya NMB wakichuana na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika mechi maalumu kwa ajili ya maadhimisho ya miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Amaan juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau Ndanda walia na Yanga

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

MCHEZO wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya wenyeji Ndanda FC ya Mtwara dhidi ya Yanga uliochezwa Mei 14, mwaka 2016 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam (sasa Benjamin Mkapa), umeibua mjadala katika kikao cha wadau wa soka waliokuwa wanajadili mwenendo wa kusuasua kwa timu yao inayoshiriki Ligi ya Championship.

Hata hivyo, kiasi cha Sh. milioni 22.5 kinatarajiwa kukusanywa kwa ajili ya kuisaidia timu hiyo itimize malengo yake ya kurejea katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mbali na mchezo huo uliopaswa kuchezwa Mtwara na baadaye kuhamishiwa Dar es Salaam baada ya Yanga kuomba kuwagharamia Ndanda katika mchezo huo, pia suala la jina la Ndanda limeelezwa kutoendana na ushiriki wa wakazi wote wa mkoa huo.

Wakichangia sababu za kusuasua kwa timu hiyo, wadau waliokutana chini ya Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, wameeleza kitendo hicho kiliwamaliza wakati kiliwapa Yanga nafasi ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara mwaka huo.

Hoja hiyo iliibuliwa na Katibu Tawala wa Wilaya ya Nanyumbu, Salum Mpalango, na kusema tangu wakati huo wadau wengi wa soka mkoani hapa walijiweka pembeni kuisaidia timu hiyo.

"Mkuu wa mkoa nikuambie ukweli Mtwara tumeathiriwa na U-simba na U-Yanga kiasi ambacho hatuipi thamani timu inayotutambulisha kisoka katika ngazi ya kitaifa, na hili tusipobadilika tutakuwa hatutoki hapa tulipo," alisema Mpalango.

Mbunge wa Nanyamba, Abdallah Chikota, alisema kitendo cha timu hiyo kukubali kuacha uwanja wake wa nyumbani wakati huo ulikuwa ni ukatili dhidi ya mashabiki na wapenda soka wa Mtwara kushuhudia bingwa wa wakati huo akimalizia mchezo wake nyumbani badala ya ugenini kama ratiba ilivyoonyesha.

Aliongeza hata jina la Ndanda 'halibebi' uhusika wa mkoa wa Mtwara hali inayowafanya wadau wengine wasiotoka Ndanda kuona timu hiyo haiwahusu.

Mwenyekiti wa Chama cha Soka Mkoa wa Mtwara (MTWAREFA), Athumani Kambi, alisema kukosekana kwa wakurugenzi ndani ya timu hiyo ni sababu nyingine inayopelekea ugumu wa kuiendesha timu.

Katibu wa Ndanda, Selemani Kachenje, alisema kwa sasa wameweka rehani gari inayomilikiwa na timu hiyo kwa ajili ya kuihudumia timu kufika katika baadhi ya vituo walivyopangiwa kucheza.

## ZISIKUPITE

### DE BEEK APATA RUHUSA

MANCHESTER United imempa ofa kiungo Mholanzi Donny van de Beek, 24, kwenda Newcastle United au Borussia Dortmund. ***(Manchester Evening News)***

### RUIZ ANUKIA UNITED

KLABU ya Manchester United ipo katika nafasi nzuri ya kumsajili kiungo wa kati wa Napoli na Timu ya Taifa ya Hispania, Fabian Ruiz, 25. ***(La Republica)***

### RASHFORD KUPEWA MKATABA

MANCHESTER United wanajipanga kumpa mshambuliaji wake, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 24 mkataba mpya msimu huu wakati wa kipindi cha majira ya joto. ***(ESPN)***

### BOWEN AITAKA LIVERPOOL

MSHAMBULIAJI wa West Ham, Jarrod Bowen, 25, anataka kuhamia Liverpool, ambayo bado ina nia ya kutaka kumnunua Mwingereza huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Football Insider)***

### CANTWELL ANUKIA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United imeongeza nia ya kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Norwich, Todd Cantwell, raia wa England, 23 . ***(Rudy Galetti - Calciomercato)***

### ARSENAL KUSAJILI SABA

ARSENAL wana orodha ya wachezaji saba wanaolengwa mojawapo akiwa ni Youri Tielemans wa Leicester mwenye umri wa miaka 24, Georginio Wijnaldum (31), wa Paris St-Germain na Bruno Guimaraes anayeichezea Lyon ambaye ana umri wa miaka 24. ***(Mirror)***

### RICO ATAKIWA VILLA

ASTON Villa imeonyesha nia ya kutaka kumsajili golikipa wa Paris St-Germain raia wa Hispania, Sergio Rico, 28. ***(Express)***

### TANNER AGEUKA LULU

KLABU za Watford, Southampton na Norwich zinamfuatilia kwa karibu winga wa Lewes, Ollie Tanner, 19. ***(Sun)***

### LOOKMAN KUBAKI LEICESTER

KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers anatumaini kufanya uhamisho wa mkopo kwa winga wa England, Ademola Lookman kutoka RB Leipzig kuwa na mkataba wa kudumu. ***(Leicester Mercury)***


### PEDERSEN AGOMBEWA ENGLAND

KLABU ya Burnley inapambana na Nottingham Forest na Coventry kwa ajili ya kumsajili mlinzi wa Birmingham na Denmark, Kristian Pedersen, 27. ***(Football Insider)***

### FRANCA AKARIBIA CITY

KLABU ya Manchester City inavutiwa na kiungo wa kati chipukizi wa Flamengo ambaye ni raia wa Brazil, Matheus Franca, 17. ***(BolaVip)***

## DOND A SOKA MAGA ULAYA



# RUDIGER KUPEWA MKATABA 'MNONO'

## ●●● Lengo ni kuhakikisha Chelsea inafanikiwa kumbakiza beki huyo ambaye pia...

**LONDON,** England

KLABU ya Chelsea inajipanga kumwandalia mkataba mpya beki wake mahiri, Antonio Rudiger ambaye mkataba wake unamalizika ifikapo mwishoni mwa msimu huu.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ujerumani tayari Januari hii yupo huru kufanya mazungumzo ya awali na klabu yoyote kabla ya kusaini mwishoni mwa msimu huu.

**Chelsea bado haijakata tamaa ya kujaribu kumbakisha mlinzi huyo ambaye anawindwa na klabu kadhaa kubwa Ulaya kama Real Madrid, Paris Saint-Germain na Juventus ambao wamepanga kumpa mkataba mnono.**

Chelsea wanajiandaa kuboresha mkataba mpya kabla hajasaini mkataba wa awali na timu yoyote.

Rudiger amekataa ofa ya mshahara wa pauni 140,000 kwa wiki kwa sababu anajua kuna klabu kubwa zimeandaa donge nono kwa ajili yake. Nyota huyo ameripotiwa anataka mshahara wa kuanzia pauni 250,000 kwa wiki ili aweze kubakia katika klabu hiyo.

Kiwango cha hivi karibuni kutoka kwa Mjerumani huyo kimemvutia kocha mkuu wa Chelsea, Thomas Tuchel na kuonekana muhimu kwenye mipango yake ya baadaye ambapo anajaribu kila liwezekano kumbakisha.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 846

MECHI KALI
ASTON VILLA
VERSUS
MANCHESTER UTD
1 | 2.79
X | 3.32
2 | 2.50

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# COUTINHO: NIMEKUJA VILLA KURUDISHA MAKALI YANGU



**LONDON,** England

KIUNGO wa Barcelona, Phillipe Coutinho aliyehamia Aston Villa kwa mkopo wa miezi sita amesema kocha wa timu hiyo, Steven Gerrard ndiye aliyemshawishi kuhamia huko ili aweze kurejesha makali yake.

Coutinho ambaye ameshindwa kupata nafasi katika kikosi cha Barcelona, amekamilisha uhamisho wake wa kuichezea Aston Villa mpaka mwisho wa msimu siku ya Jumanne huku kukiwa na kipengele cha kumnunua moja kwa moja kwa kiasi cha pauni milioni 33 kipindi cha majira ya joto.

Akielezea uamuzi wake wa kuhamia Aston Villa, Coutinho aliiambia BBC Sport: "Steven Gerrard aliniambia kuhusu klabu, shauku na mipango ya yake kwenye klabu.

"Nilipozungumza naye baada ya kikao ilikuwa wazi anataka nije hapa, nadhani imekuwa haraka na nafurahi kuwa hapa.

Coutinho alikuwa anahitaji kurudi katika Ligi Kuu England na kucheza mara kwa mara na aliona Aston Villa kama klabu sahihi ambayo inaweza kutengeneza kitu kizuri hapo baadaye.



## Arteta akataa kumuuza Nketia

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amekanusha uwezekano wa Eddie Nketiah kuihama klabu hiyo katika dirisha la usajili la Januari.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 yupo katika miezi sita ya mwisho ya mkataba wake hapo kwenye Uwanja wa Emirates na anaaminika kuwa kwenye mazungumzo ya kuhamia Crystal Palace.

Mara baada ya mechi ya kwanza ya nusu fainali ya Kombe la EFL dhidi ya Liverpool juzi ambayo ilimalizika kwa sare ya bila kufungana, Arteta alisisitiza nyota huyo raia wa England hataelekea kwingine wakati wa majira haya ya baridi.

"Hali ni kwamba Eddie ni mchezaji wetu na atabakia hapa kwetu. Ni mchezaji wetu na yuko chini ya mkataba, kwa hivyo atakuwa nasi," alisema Arteta aki- waambia waandish habari

Nketiah amefunga tano kwenye mechi Kombe la EFL msin 2021-22, lakini am dakika 38 pekee k Ligi Kuu England huu.

Kinda huyu wa Uin anajivunia jumla y bao 18 na asisti moja mechi 72 akiwa na A akitokea katika ak yao.

,297,200

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 15/01/22 | 18:00 | Mallorca vs Espanyol | 2.50 | 2.94 | 2.99 |
| 02. 15/01/22 | 18:15 | OH Leuven vs Mechelen | 2.31 | 3.49 | 2.81 |
| 03. 15/01/22 | 18:30 | Boavista vs Gil Vicente | 2.87 | 3.12 | 2.46 |
| 04. 15/01/22 | 20:30 | Monchengladbach vs Bayer Leverkusen | 2.54 | 3.69 | 2.49 |
| 05. 15/01/22 | 20:30 | Sporting Gijon vs Cadiz CF | 2.50 | 2.99 | 2.94 |
| 06. 15/01/22 | 20:30 | Girona vs Rayo Vallecano | 2.52 | 3.11 | 2.81 |
| 07. 15/01/22 | 20:45 | NEC Nijmegen vs Heracles Almelo | 2.35 | 3.29 | 2.85 |
| 08. 15/01/22 | 21:00 | Nancy vs Bastia | 2.70 | 3.09 | 2.60 |
| 09. 15/01/22 | 21:00 | US Quevilly Rouen vs Amiens | 2.81 | 3.20 | 2.43 |
| 10. 15/01/22 | 23:30 | Betis vs Sevilla FC | 2.57 | 3.16 | 2.71 |
| 11. 16/01/22 | 16:30 | Cambuur vs Sparta Rotterdam | 2.37 | 3.49 | 2.70 |
| 12. 16/01/22 | 17:00 | Lorient vs Angers | 2.37 | 3.19 | 3.04 |
| 13. 16/01/22 | 18:00 | Eupen vs Cercle Brugge | 2.95 | 3.35 | 2.28 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 15/01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 5505 | Kariobangi Sharks vs AFC Leopards | 2.39 | 3.00 | 3.25 |
| 15:30 | 3805 | Manchester City vs Chelsea | 1.75 | 3.74 | 4.51 |
| 15:30 | 4149 | Luton Town vs Bournemouth | 2.90 | 3.29 | 2.32 |
| 15:30 | 4826 | Cardiff vs Blackburn | 2.55 | 3.23 | 2.65 |
| 16:00 | 5821 | Sivasspor vs Trabzonspor | 3.01 | 3.16 | 2.35 |
| 17:00 | 5055 | Sampdoria vs Torino | 2.89 | 3.24 | 2.46 |
| 17:30 | 2027 | FC Koln vs Bayern Munchen | 6.98 | 5.78 | 1.34 |
| 17:30 | 2429 | VfL Wolfsburg vs Hertha BSC | 1.99 | 3.48 | 3.63 |
| 17:30 | 3191 | Union Berlin vs Hoffenheim | 2.78 | 3.52 | 2.38 |
| 17:30 | 3421 | Mainz vs VfL Bochum | 1.70 | 3.77 | 4.76 |
| 17:30 | 4821 | Stuttgart vs RB Leipzig | 4.89 | 4.19 | 1.61 |
| 18:00 | 1629 | Huddersfield vs Swansea | 2.60 | 3.14 | 2.65 |
| 18:00 | 1705 | Millwall vs Nottingham | 2.23 | 3.14 | 3.19 |
| 18:00 | 2448 | Middlesbrough vs Reading | 1.46 | 4.13 | 6.48 |
| 18:00 | 2803 | QPR vs West Bromwich | 3.25 | 3.34 | 2.11 |
| 18:00 | 3003 | Mallorca vs Espanyol | 2.50 | 2.94 | 2.99 |
| 18:00 | 3236 | Peterborough vs Coventry | 3.14 | 3.33 | 2.17 |
| 18:00 | 3318 | Newcastle vs Watford | 2.05 | 3.60 | 3.40 |
| 18:00 | 3380 | Wolverhampton vs Southampton | 2.28 | 3.15 | 3.30 |
| 18:00 | 3908 | Derby vs Sheffield Utd | 3.30 | 3.15 | 2.18 |
| 18:00 | 4093 | Fulham vs Bristol City | 1.20 | 6.11 | 11.83 |
| 18:00 | 4393 | Preston vs Birmingham | 1.98 | 3.34 | 3.63 |
| 18:00 | 5794 | Burnley vs Leicester | 2.91 | 3.36 | 2.39 |
| 18:00 | 5813 | Dunfermline vs Hamilton | 2.79 | 3.23 | 2.40 |
| 18:15 | 3164 | Lamia vs Ionikos Nikea FC | 2.15 | 3.11 | 3.46 |
| 18:15 | 3789 | OH Leuven vs Mechelen | 2.09 | 3.65 | 3.10 |
| 18:15 | 5440 | Asteras Tripolis vs Volos | 1.78 | 3.40 | 4.53 |
| 18:30 | 2578 | Boavista vs Gil Vicente | 2.96 | 3.10 | 2.41 |
| 19:00 | 1425 | Nigeria vs Sudan | 1.22 | 5.35 | 15.86 |
| 19:00 | 1432 | Antalyaspor vs Fenerbahce | 3.35 | 3.40 | 2.07 |
| 19:00 | 1720 | St Etienne vs Lens | 3.68 | 3.53 | 1.96 |
| 20:00 | 4592 | Salernitana vs Lazio | 6.36 | 4.57 | 1.46 |
| 20:30 | 1363 | Apollon Smyrnis vs Aris Salonica | 3.94 | 3.40 | 1.90 |
| 20:30 | 2515 | Girona vs Rayo Vallecano | 2.45 | 3.10 | 2.90 |
| 20:30 | 2758 | Monchengladbach vs Bayer Leverkusen | 2.53 | 3.78 | 2.46 |
| 20:30 | 2793 | PAOK vs OFI Crete | 1.34 | 4.73 | 8.48 |
| 20:30 | 4096 | Sporting Gijon vs Cadiz CF | 2.39 | 3.00 | 3.10 |
| 20:30 | 4425 | Aston Villa vs Manchester Utd | 2.79 | 3.32 | 2.50 |
| 20:30 | 5937 | RFC Seraing vs Union Saint Gilloise | 7.30 | 4.93 | 1.36 |
| 20:45 | 1074 | NEC Nijmegen vs Heracles Almelo | 2.43 | 3.29 | 2.75 |
| 21:00 | 4846 | Benfica vs Moreirense | 1.17 | 6.70 | 13.79 |
| 22:00 | 1782 | Twente vs Heerenveen | 1.78 | 3.69 | 4.04 |
| 22:00 | 2335 | Guinea Bissau vs Egypt | 8.73 | 4.07 | 1.41 |
| 22:00 | 2584 | Feyenoord vs Vitesse Arnhem | 1.40 | 4.71 | 6.47 |
| 22:45 | 2232 | Brugge vs St Truiden | 1.26 | 5.72 | 9.27 |
| 22:45 | 5242 | Juventus vs Udinese | 1.45 | 4.30 | 7.30 |
| 23:00 | 1272 | Paris St Germain vs Brest | 1.25 | 6.06 | 9.80 |
| 23:00 | 3114 | GO Ahead Eagles vs Waalwick | 2.07 | 3.43 | 3.28 |
| 23:30 | 3176 | Betis vs Sevilla FC | 2.52 | 3.11 | 2.81 |
| 23:30 | 3857 | GD Estoril vs FC Arouca | 1.77 | 3.45 | 4.53 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# DODOMA JIJI YAITISHA GEITA GOLD LIGI KUU

**Na Dennis Fusi**

LIGI Kuu ya NBC Tanzania Bara inatarajiwa kuendelea tena leo kwa Dodoma Jiji FC kuwakaribisha Geita Gold kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

**Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji, Mbwana Makata, aliliambia gazeti hili kikosi chake kiko tayari kwa ajili ya mchezo huo na wamejipanga kuzibakisha pointi tatu nyumbani.**

Makata alisema wanafahamu watakutana na timu ngumu ambayo imejiimarisha katika dirisha dogo, lakini hawana hofu yoyote kuhusiana na mechi hiyo.

"Tuko tayari kwa mechi hii dhidi ya Geita Gold, tunajua tunaanza safari ya kuelekea lala salama, kila mechi itakuwa ngumu na yenye ushindani, tucheze nyumbani au ugenini, tumejiandaa kupambana," alisema Makata.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya wenyeji Biashara United dhidi ya Kagera Sugar.

Tayari kikosi cha Kagera Sugar kinachonolewa na Mkenya Francis Baraza kimeshawasili Musoma kwa ajili ya mchezo huo utakaochezwa kwenye Uwanja wa Karume mkoani Mara.

"Sisi kila mechi kwetu ni muhimu, tunawaheshimu Biashara United kwa sababu ina wachezaji wazuri na wanaojituma, wamecheza mashindano ya kimataifa na kupata uzoefu zaidi, tunajua haitakuwa mechi rahisi kwa timu zote mbili," Baraza alisema.

Simba ndio mabingwa watetezi wa ligi hiyo wakati Yanga yenye pointi 29 wako kileleni katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali.



Washiriki wa Semina ya Maendeleo ya Ligi inayoendeshwa na mpango wa UEFA Assist wakimsikiliza mkufunzi wao (hayupo pichani), akitoa maelekezo kwenye hoteli ya Golden Tulip jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: TFF**

# Mtibwa Sugar yaikera Simba SC

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Simba wakiibuka mabingwa wapya wa mashindano ya Kombe la Mapinduzi mwaka huu, Mtibwa Sugar imeweka video fupi katika mtandao rasmi wa klabu hiyo ikionyesha mechi ya fainali iliyowakutanisha na vigogo hao wa soka nchini dhidi ya 'Wakata Miwa' hao mwaka 2020 ambapo walishinda bao 1-0.


Ilikuwa ni Januari 13, 2020 mfungaji wa bao pekee katika fainali hiyo alikuwa ni Awadh Salum, akifunga goli hilo dakika ya 38 , lakini video hiyo ikasababisha 'povu' kutoka kwa baadhi ya mashabiki wa Simba wakisema ilikuwa ni kijembe kwao.

"Tarehe kama ya leo 2020, Awadh Juma alitufungia bao dhidi ya Simba, Visiwani kwenye fainali ya Mapinduzi Cup na kupekelea kuwa mabingwa wa michuano hiyo. Unakumbuka nini katika mchezo huu?" iliandika klabu hiyo.

Mashabiki wa Simba walijibu kuonyesha hisia zao, wakidai Mtibwa Sugar ilikuwa ikiwapiga madogo, lakini baadhi wakitaka mwakani timu hiyo kupewa nafasi ya kushiriki michuano hiyo kwa sababu ina mashabiki wengi Zanzibar.

Baadhi walisema wanachokumbuka ni kujiuzulu kwa aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Simba, Mohamed Dewji kwenye wadhifa wake huo, akionekana kukerwa na matokeo hayo, ingawa baadaye alibadili uamuzi.

Simba imeshinda taji hilo lililoachwa na Yanga baada ya kuifunga Azam FC bao 1-0, shukrani Meddie Kagere aliyepachika goli hilo katika mchezo huo kwa penalti.



ah

ni wa

a mara
tatu za
mu wa
echeza
wenye
msimu

gereza
a ma-
katika
Arsenal
kademi

# Michezo

Jumamosi Januari 15, 2022

Nipashe




Rudiger kupewa mkataba 'mnono'

UKURASA 21



Mashabiki wa Simba waliojitokeza kuipokea timu yao baada ya kushinda ubingwa wa mashindano ya Kombe la Mapinduzi 2022 wakigombania kulishika kombe walilotwaa katika mechi ya fainali dhidi ya Azam FC iliyochezwa kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar juzi. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Yanga Sc, Coastal Union zatishana

**Na Adam Fungamwango**

IKIWA imebaki siku moja tu kabla ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga kati ya wenyeji Coastal Union dhidi ya Yanga kutoka Dar es Salaam, kila upande umetamba kuibuka na ushindi katika mchezo huo.

Yanga itaingia kwenye uwanja huo ikiwa haijashinda mechi yoyote ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Wagosi wa Kaya hayo kwa misimu saba.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli aliliambia gazeti hili kwa sasa wao hawaishi kwa historia wala rekodi, na siku zote 'kuti la mazoea' ndilo humwangusha mgema.

Bumbuli alisema Coastal Union kwa sasa wamekuwa wakiishi maisha ya kukariri na historia, kitu ambacho wao hawakiamini, hivyo watashuka kwenye uwanja huo kusaka matokeo ya ushindi bila kufikiria matokeo mabaya wanayoyopata kwenye uwanja huo.

Katibu Mkuu wa Coastal Union, Rashid Mgwemo alisema ana uhakika wa kuibuka na ushindi kutokana na historia yao nzuri wanapocheza dhidi ya Yanga nyumbani kwao.

"Mechi itakuwa nzuri na ngumu. Sio siri kuwa Yanga msimu huu ni nzuri na ina wachezaji wazuri, lakini ikumbukwe msimu uliopita tuliwafunga Mkwakwani, tukiwa hatuna timu nzuri kama msimu huu. Kwa hiyo na sisi msimu huu tuna timu nzuri kuliko hata ya msimu uliopita, waje vizuri tu," Mngweno alionya.

# CHAMA: NIMERUDI NYUMBANI

## ●●● Kiungo huyo afunguka siri iliyosababisha kufanya uamuzi wa...

**Na Saada Akida,** ZANZIBAR

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco akiwapongeza wachezaji wake kwa kufuta historia ya kupoteza mechi ya fainali ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi Zanzibar, kiungo Mzambia Clatous Chama amesema amerejea nyumbani.

Simba ilimtangaza rasmi Chama amerejea kwa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara jana akitokea RS Berkane ya Morocco ambayo ilimnunua kiungo huyo mwaka jana.

Chama, nyota anayekipiga pia katika Timu ya Taifa ya Zambia (Chipolopolo), alisema anaamini ujio wake utaisaidia Simba kufikia malengo kwa sababu kwa sasa uwezo na uzoefu wake umeongezeka.

"Mwenda kwao si mtoro," alisema kwa kifupi Chama baada ya kutangazwa amerejea Msimbazi.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah, aliliambia gazeti hili wamejipanga kuendelea kuiimarisha timu hiyo ili ifanye vizuri zaidi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, michuano ya Kombe la FA na mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika wanayoshiriki.

Salim alisema wamefanya usajili huo kwa kuzingatia mahitaji halisi na ripoti iliyowasilishwa na benchi la ufundi la timu hiyo pekee nchini iliyobakia kwenye michuano ya kimataifa.

**"Mashabiki wanatakiwa kuwa watulivu kwa sababu ndaniya hizi siku mbili tutaweka waz i usajili tuliofanya katika diri sha dogo, lakini pia tumeweka mipango yetu sawa kuhakiki sha tunafanya vizuri katika kila michuano iliyopo mbele yetu," alisema kiongozi huyo.**

Alisema timu yao imekuwa na mabadiliko makubwa na wachezaji wanacheza mpira 'biriani' ambao walikuwa wakicheza msimu uliopita.

Akizungumza na gazeti hili jana, Pablo alisema anawapongeza wachezaji wake kwa kupambana katika muda wote wa mechi hiyo ya fainali na hatimaye kutimiza malengo yao ya kulichukua kombe hilo mwaka huu.

Pablo alisema mchezo ulikuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa, lakini pia anawapongeza wachezaji wa Azam FC kwa kucheza mpira mzuri ambao lengo lake ilikuwa ni kupata matokeo chanya ambayo kwao yalikosekana.

"Sasa tumemaliza Mapinduzi na tunarejea katika Ligi Kuu, tutahakikisha tunafanya vizuri katika michezo yetu ijayo kwa kucheza soka safi kama ilivyokuwa kwenye michuano ya Mapinduzi," alisema Pablo.

Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere ambaye aliibuka Mfungaji Bora wa mashindano hayo alisema anafurahi kupata tuzo hiyo na kuongeza si uwezo wake binafsi bali ni ushirikiano mzuri alioupata kutoka kwa wachezaji wenzake wa timu hiyo.

Kagere alisema kazi yake kubwa ni kufunga na ataendelea kufanya hivyo kila atakapopata nafasi ili kufikia malengo yao ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano mingine inayowakabili.

"Tumemaliza Mapinduzi, sasa akili na nguvu zetu zote zinaelekezwa katika Ligi Kuu, tunaenda kupambana ili kupata matokeo mazuri katika kila mechi tutakayocheza," alisema Kagere.

Tayari mabingwa hao wa Kombe la Mapinduzi wamesharejea Dar es Salaam tangu jana na wanajipanga na leo wanaanza mikakati ya kuelekea Mbeya kwa ajili ya kukutana na Mbeya City hapo keshokutwa kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya.

Mbali na kutwaa ubingwa wa Kombe la Mapinduzi, tuzo nyingine zilizochukuwa na nyota wa Simba ni ya Mchezaji Bora wa michuano hiyo ni Pape Sakho, Golikipa Bora ni Aishi Manula na Mchezaji Bora wa mechi ya fainali ni Henock Ibanga.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, SL P 31042

9 770856 541002 >